**Ujumbe** wa TEC Kwaresma una hoja nzito kwa familia, kisiasa

UKURASA 5



**Uchunguzi** waanza tena mitihani ya Shule ya Sheria

UK. 8

**Mtoto** wa miaka 8 anyongwa, mwili wakutwa kwenye kichaka shuleni

UKURASA 9


Makonda anavyogeuka kuwa mtetezi wa watu

siasa

Demokrasia ya makundi CCM ilishia kwa Lowassa

WAKATI MISWADA IKIMSUBIRI RAIS

Wadau: Marekebisho yamejaa mwingiliano wa katiba, sheria

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Februari 14, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581586

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Warioba: Nilimshauri Lowassa aachie ngazi




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiongoza waombolezaji kuaga mwili wa Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa katika viwanja vya Karimjee, Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

- **Lissu**, Rostam, Shein waanika mapya mengine ... *Endelea Ukurasa 2, 3 & 7*

**"Nikamwambia (Lowassa) haya ni mambo ya kisiasa hata kama wangekusikiliza, kwa hali iliyokuwapo, ilibidi uachie ngazi kwa sababu nguvu zako zilikuwa zimeshapunguzwa."**
WARIOBA

**"Lowassa alikuwa mwanasiasa mwenye ushawishi katika siasa za Tanzania kuliko mwanasiasa mwingine tangu kufariki dunia kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere."**
LISSU

**Lowassa hakuhama CCM kwa sababu ya kutofautiana kiitikadi na chama chake bali hakutendewa haki na alitaka kutuma ujumbe kwamba lazima hali ibadilike."**
ROSTAM

## Makonda anyooshewa kidole kauli kuhusu haki mahakamani

UKURASA 4



## Uongezaji makalio Muhimbili waibua mvutano bungeni

UKURASA 4

## Mawaziri wawili wa JK wafariki dunia

UKURASA 5

MICHEZO GAMONDI AISHTUKIA SIMBA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Warioba: Nilimshauri Lowassa aachie ngazi

**Na Jenifer Gilla**

MWANASHERIA na mwanasiasa mkongwe, Jaji Joseph Warioba, ameeleza alivyomshauri Edward Lowassa, kuhusu kujiuzulu nafasi ya Waziri Mkuu.

Jaji Warioba ambaye aliwahi kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mwaka 1985 hadi 1990, aliyasema hayo jana wakati akitoa salamu za pole wakati wa kuuaga mwili wa Lowassa katika viwanja vya Karimjee, Dar es Salaam.

Lowassa alijiuzulu katika nafasi hiyo mwaka 2008 kutokana na kashfa ya zabuni ya kufua umeme wa dharura iliyopewa kampuni ya Richmond, baada ya kuitumikia kwa takriban miaka miwili tangu alipoteuliwa na rais wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete.

Warioba alisema alisikia taarifa za kujiuzulu kwa Lowassa bungeni wakati akiwa Dar es Salaam kuwa hakutendewa haki kwa kuwa walimhukumu bila ya kumsikiliza.

Alisema aliposikia taarifa na malalamiko hayo alitoa tamko kuwa kama kweli wamemtuhumu Waziri Mkuu bila kumsikiliza, hawakumtendea haki.

Hata hivyo, alisema baada ya muda, Lowassa alimtafuta kwa ajili ya kumpa malalamiko hayo na alisisitiza kuwa bado ilikuwa muhimu kwake kujiuzulu hata kama angepewa nafasi ya kusikilizwa kutokana na hali ilivyokuwa.

"Bado nikamwambia haya ni mambo ya kisiasa hata kama wangekusikiliza kwa hali iliyokuwapo, ilibidi uachie ngazi kwa sababu nguvu zako zilikuwa zimeshapunguzwa," alisema.

Mamia ya waombolezaji jana walijitokeza katika viwanja hivyo kutoa salamu za mwisho kwa mwili wa kiongozi huyo aliyefariki dunia Februari 10, mwaka huu, saa 8:00 mchana katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) alikokuwa akipatiwa matibabu.

**HALI KARIMJEE**

Mpaka kufikia saa 4:00 asubuhi, viwanja hivyo vilikuwa vimefurika mamia ya waombolezaji wakiongozwa na Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na viongozi mbalimbali wa serikali na vyama vya siasa.

Mwili wa marehemu uliingia katika viwanja hivyo saa 4: 20 asubuhi ukiwa umepakiwa katika gari maalum la Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kisha ulipelekwa kwenye jukwaa na maofisa wa jeshi hilo kwa mwendo wa pole wakisindikizwa na mapigo ya tarumbeta.

Wakati mwili ukielekezwa kwenye jukwaa, watu wote walisimama ukimya ulitawala kila mmoja akitafakari mambo makubwa aliyoyashuhudia au kujifunza kutoka kwa kiongozi huyo.

Baada ya mwili kuwekwa mahali palipoandaliwa, zilifuata sala fupi kutoka kaa viongozi wa dini na madhehebu mbalimbali kisha salamu za rambirambi kutoka kwa viongozi.




Mjane wa Hayati Edward Lowassa, Regina Lowassa, akiiongoza familia kuuga mwili wa mpendwa wao katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

Saa 6:20 mchana, Makamu wa Rais Mpango na viongozi wengine wa serikali na familia ya marehemu, waliongoza Watanzania kutoa salamu za mwisho kwa kiongozi huyo, shughuli iliyochukua takribani saa mbili.

Akitoa salamu za pole kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, Dk. Mpango aliwasihi viongozi wa serikali na Watanzania kumuenzi Lowassa kwa kuyaendeleza mazuri aliyokuwa akiyafanya kwa maendeleo ya nchi.

Dk. Mpango alisema serikali itamkumbuka kama kiongozi aliyejitoa kwa dhati na kutumia karama aliyopewa na Mwenyezi Mungu kuwatumikia Watanzania.

Alisema maisha ya kiongozi huyo yameacha mafunzo mengi ikiwamo uchapakazi hodari katika chama, utumishi wa umma na shughuli binafsi kama vile ufugaji.

"Kwa hivyo inatupasa Watanzania kumuenzi kwa kuchapa kazi ili kuboresha maisha yetu na kuchangia katika ujenzi wa taifa," alisema.

Pia aliwasihi viongozi wajifunze kutoka kwa Lowassa kwa kutetea maslahi ya taifa kwa kuwa kiongozi huyo alikuwa mtetezi wa maslahi ya wananchi wa Jimbo la Monduli katika kipindi chote alichowahudumia akiwa mbunge.

Aliwakumbusha pia viongozi wa sasa na wa baadaye kuiga mfano wa marehemu kwa kuwa na uthubutu wa kubuni miradi mikubwa yenye kuiletea nchi maendeleo. Alitoa mfano wa alipokuwa Waziri wa Maji na Mifugo alibuni miradi ya kuboresha huduma ya maji kwa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria.

Jambo lingine, kwa mujibu wa Dk. Mpango ni suala la elimu alilolipa kipaumbele na mara zote alipoulizwa vipaumbele vyake, alitaja elimu katika nafasi ya kwanza hadi ya tatu na kwa sababu hiyo alisimamia kwa uhodari utekelezaji wa sera, mikakati na mipango ya elimu ikiwamo ujenzi wa shule za sekondari za kata.

"Kwa hiyo Watanzania wote hasa vijana yatupasa tumuenzi Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kutumia fursa mbalimbali kujipatia elimu kwa manufaa yetu na taifa," alisisitiza.

Pia alisema alikuwa mwana mazingira hodari, alihimza na kuongoza kampeni za uhifadhi wa mazingira na kuwakumbusha Watanzania kumuezi hasa katika kutunza vyanzo vya maji ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema serikali inaiombea familia faraja, na kumwomba mjane, familia na Watanzania kuupokea msiba huo kwa imani na kudumisha amani na upendo kwa manufaa ya nchi.

**WASAFIRI KUMUAGA**

Kikundi cha watu 15 wa jamii ya wafugaji wa kabila la Wamasai kutoka Mvomero mkoani Morogoro, wamesafiri hadi Dar es Salaam kumuaga kiongozi huyo.

Walisema kufika kwao kuuaga mwili wa Lowassa ambaye alikuwa mstari wa mbele katika kutetea watu wa jamii hiyo ni kutoa shukrani kwa kuwa aliwapa mwongozo katika mambo mengi ya maendeleo.

Mwakilishi wa kundi hilo, Thomas Mgema, alisema wamepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Lowassa kwa kuwa aliwapigania na kuwaelimisha na kuwapa umuhimu wa elimu.

"Alikuwa akija kule tunakoishi kipaumbele cha kwanza alikuwa anatuambia twende shule na sasa katika jamii yetu wengi wamesoma," alisema Mgema.

Rudia Kamando alisema wamepoteza mtu muhimu katika maisha yao kwa kuwa aliwapigania sana watu wa jamii hiyo katika elimu na mambo mengine ya kimaendeleo.

DRC Danish Refugee Council
P.O Box 177
Old IRC Road
Kibondo, Kigoma
Tanzania
T: +255 282 820 163
EAGL-info@drc.ngo
www.drc.ngo

DRC DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISH LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA HUDUMA MBALIMBALI KAMA IFUATAVYO;

- UANDAAJI NA UCHAPISHAJI (PRINTING OF VISIBILITY ITEMS)
- VIFAA VYA MATUMIZI YA OFISI
- VIPURI VYA MAGARI NA BAJAJI
- MAJI YA KUNYWA
- PEMBEJEO ZA KILIMO
- VIFAA VYA UJENZI
- VIFAA VYA MATUMIZI YA NYUMBANI
- HUDUMA ZA MALAZI NA KUMBI ZA MIKUTANO

HIVYO SHIRIKA LA DANISH LINATANGAZA ZABUNI TAJWA HAPO JUU NA WAZABUNI WAFUATE MAELEKEZO YAFUATAYO.

- USITUMIE WINO WA MAJI KUSAHIHISHA UNAPOFANYA KOSA.TUMIA KARATASI MPYA
- USIBADILISHE KARATASI ZA ZABUNI KWENDA KWENYE MFUMO WORD/EXCEL,
- ZINGATIA SEHEMU ZA KUSAINI NA KUGONGA MUHURI AMBAZO NI LAZIMA
- USISAHAU KUAMBATANISHA NYARAKA ZINAZOHITAJIKA KAMA ZILIVYOAINISHWA. BAADA YA KUMALIZA SEHEMU ZOTE SAINI, GONGA MUHURI, WEKA TAREHE.

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAALIKA WAZABUNI KUWASILISHA MAOMBI YAO YA UZABUNI.

NYARAKA HUSIKA ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 14.02.2024 HADI TAREHE 27.02.2024 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA **+255 653 468 638** au BARUA PEPE **joram.nshatsi@drc.ngo**

UNAPASWA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA BARUA PEPE: **rfq.tza@drc.ngo** AU KULETA MOJA KWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
12.02.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **15.02.2024 hadi 21.02.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Bandari ya Dar Es Salaam kuelekea Mzenga,** gari hilo lenye namba za usajili **NRB97300 / NRB15200 DS00TG GP / NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.50** |
| **Upana** | - | **Mita** | **7.40** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.70** |

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar Es Salaam hadi Mzenga** kupitia **Barabara ya Mandela,** Barabara ya **Morogoro mpaka Mlandizi,** magari yatasafiri muda wa usiku ***( Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri).*** Kutoka Mlandizi kwenda Mzenga magari yatasafiri muda wa mchana ***( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117835802

## HABARI KITAIFA




Askari wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa Hayati Edward Lowassa, baada ya kuwasili katika viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rostam afichua kilichompeleka Lowassa upinzani

**Na Elizabeth Zaya**

MFANYABIASHARA maarufu, Rostam Aziz, ameeleza sababu za aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwenda Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kugombea nafasi ya urais.

Amesema mwanasiasa huyo aliyefariki dunia Jumamosi iliyopita, hakufanya hivyo kwa sababu ya kutofautiana kiitikadi na chama chake bali hakutendewa haki na alitaka kutuma ujumbe kwamba lazima hali ibadilike.

Alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akimzungumzia Lowassa alivyomfahamu na alivyokuwa naye karibu katika masuala mbalimbali yaiwamo ya kisiasa walipokuwa wote bungeni.

Rostam ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Igunga kwa vipindi kadhaa, alisema baada ya ujumbe huo kuwa umetumwa na kwamba ndani ya CCM watu wameelewa kwa nini alifanya hivyo, Lowassa hakuwa na tatizo la kurudi alikotoka (CCM) kwa sababu ndiko kulikuwa nyumbani kwake.

"Lowassa alitoka CCM kwenda kugombea nafasi hiyo (urais) kupitia upinzani kwa sababu kuu moja, alikwenda upinzani kwa sababu hakutendewa haki na alitaka kutuma meseji kwamba lazima hali ibadilike," alisema.

"Siku zote tunamkumbuka kwamba yeye alikuwa mtu shujaa, alikuwa mtu wa msimamo akiamini katika haki na kwamba unapotafuta haki inawezekana ukatumia njia nyingine kuitpata," alisema.

Rostam alisema aliishi na Lowassa nyumba moja kwa miaka 15 jijini Dodoma na kwamba alikuwa akimfahamu vizuri kuliko wengine wengi.

"Nimeishi na Edward Lowassa nyumba moja Dodoma kwa miaka 15. Alikuwa kiongozi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mwenye akili tulivu, mcha Mungu wa dhati, mnyenyekevu na mwenye kauli thabiti.

"Nidhamu ndiyo jambo linalotofautisha umahiri wa Edward na wengine wengi. Taifa limepoteza kiongozi mzalendo mwenye mapenzi ya kweli kwa nchi yake," alisema Rostam.

**LISSU ANENA**

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, alisema Lowassa alikuwa mwanasiasa mwenye ushawishi katika siasa za Tanzania kuliko mwanasiasa mwingine tangu kufariki dunia kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

"Na nikisema ushawishi wa siasa sina maana ya vyeo, nina maana ya kuwa na 'political influence' (ushawishi kisiasa). Sasa Lowassa alikuwa 'perhaps the most influential figure.

"Wanasiasa wengine wote mnaowafikiria ukimwacha Baba wa Taifa, wengine wote walikuwa na ushawishi kwa sababu ya vyeo vyao. Waziri Mkuu Lowassa hakuwahi kuwa Rais, Uwaziri Mkuu wake ulikuwa wa miaka miwili tu lakini ushawishi wake katika siasa za nchi hii ulikuwa mkubwa sana," alisema.

Lissu alisema kuondoka kwake ni pigo kubwa na kwamba taifa limepoteza mwanasiasa wake maarufu.

"Nchi hii imepoteza mwanasiasa wake maarufu na mahitaji kama sehemu ya kumuenzi tunahitaji kutambua huo ushawishi wake wa kisiasa. Sisi (CHADEMA) alikuwa mgombea wetu wa urais mwaka 2015 na kwa rekodi zilizopo ambazo hakuna anayeweza kuzibisha, hakuna mwanasiasa, mgombea urais wa upinzani wa kabla yake au wa baada yake aliyepata kura nyingi za urais au aliyepata wabunge wengi kuliko Mzee Lowassa.

"Na hiyo inakuambia ni jinsi gani ambavyo alikuwa na ushawishi. Nimekuja hapa kutambua mchango wake katika maisha yetu kama taifa na pia kuwapa faraja familia yake. Mama Lowassa alikuwa mwalimu wangu nilipokuwa kidato cha kwanza miaka 41 iliyopita. Kwa hiyo nimekuja kumpa pole mwalimu wangu na familia yake," alisema.

**SUMAYE**

Waziri Mkuu mstaafu, Fredrick Sumaye, alisema Watanzania walimfuata Lowassa alipohamia upinzani kwa sababu ya ushawishi wake.

Sumaye akiwa ni miongoni mwa waliohamia upinzani katika kipindi hicho ambacho Lowassa alihamia CHADEMA, alisema kiongozi huyo enzi za uhai wake alikuwa mtu wa misimamo katika kusimamia jambo aliloliamini.

"Alikuwa akisema jambo lake analisimamia kweli na hataki mishindo. Alikuwa mchapakazi sana na kipenzi kwa Watanzania ndiyo maana alipotoka CCM kwenda upinzani walimfuata. Tumepoteza kiongozi muhimu sana," alisema Sumaye.

Naye Hamisi Mngeja, miongoni mwa watu waliomfuata Lowassa alipohamia upinzani, ambaye uamuzi wa kwenda upinzani ilikuwa ndoto na maono yake katika kulitumikia taifa.

"Katika siasa kuna wakati mnaweza kutofautiana kabisa lakini baadaye mnaweza kurudi mkawa kitu kimoja. Uamuzi wa Lowassa kwenda upinzani haukuwa mdogo, ulikuwa mgumu sana, lakini yeye alikuwa na ndoto na maono katika kulitumikia taifa," alisema Mngeja.

# Mwinyi asema Tanzania imepata pigo

**Na Jennifer Gilla**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Tanzania imepata pigo kubwa kutokana na kifo cha Waziri Mkuu Mstaafu Edward Lowassa kwa sababu mbalimbali kwa aliyoyafanya kwa taifa. Akizungumza wakati wa hafla ya kuaga mwili wa kiongozi huyo viwanja vya Karimjee, Dar es Salaam, Dk. Mwinyi alisema kwa kipindi alichofanya kazi na Lowassa, alijifunza uzalendo, uwajibikaji, ushirikiano na watu mbalimbali na kuweka mbele maslahi ya nchi.

Alisema kutokana na mambo aliyoyafanya ambayo ni alama ya kudumu katika historia ya nchi, namna bora ya kumuenzi ni kuendelea kuyaishi maono yake ya uzalendo na uwajibikaji ili kupiga hatua na kuleta maendeleo.

Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alisema taifa linapaswa kumshukuru Mungu kwa muda aliowajaalia kuishi na kiongozi huyo kwa kuwa ameacha alama zitakazokumbukwa daima.

Waziri Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye, alisema Lowassa ameacha mambo mengi ambayo watayakumbuka serikalini, kwenye chama na katika jamii hata baada ya kustaafu. Alimtaja kuwa alikuwa mchapakazi, aliyekuwa tayari kutoa ushauri wakati wowote na alitekeleza yale aliyokabidhiwa na viongozi wake na ameishi maisha ya kutukuka. Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, katika salamu zake, alisema kwa kipindi alichofanya kazi naye, alimfahamu kama mwenye juhudi katika kazi, weledi, heshima kwa kila mtu na alijitoa mhanga kwa ajili ya nchi yake.

Alisema pia alikuwa kiongozi aliyependa kujifunza muda wowote kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi yake.

**FAMILIA YATOA NENO**

Akizungunza kwa niaba ya familia, mtoto wa marehemu na Mbunge wa Monduli, Fred Lowassa, alimshukuru Rais Samia kwa kupambana kupigania afya ya baba yao katika kipindi chote cha kuuguza na kwamba vinginevyo, asingefika hata Februari 10 (tarehe aliyofariki dunia).

Aliwashukuru pia Watanzania na viongozi wote kwa kuwashika mkono katika kipindi hicho kigumu. Fred alisema msiba huo ni wa Watanzania wote kwa kuwa baba yao alikuwa mlezi na mzazi wa watu wote na alipigania kuboresha maisha ya wote ikiwamo kujenga shule za kata, kuboresha huduma ya maji na Chuo Kikuu cha Dodoma. Alisema walipokea taarifa za kifo cha baba yao kwa amani kwa kuwa aliugua kwa muda mrefu na sasa umefika muda wake wa kupumzika.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Azania Front, Joseph Mlaki, aliwasihi waombolezaji kuwa na amani mioyoni mwao kwa sababu Lowassa ameitwa na Mungu.

Mchungaji Mlaki aliwasihi pia wanafamilia na serikali kumshukuru Mungu kwa uhai wa Lowassa kwa kukaa naye kulea watoto hadi wajukuu, lakini pia wakipata nafasi ya kumuuguza hadi umauti kumkuta.


**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA CNBMI TANZANIA LIMITED**

**Cheti cha Usajili No. 127673**

**Sheria ya Makampuni, 2002 (Kifungu 334 (1))**

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni **CNBMI TANZANIA LIMITED,** yenye usajili namba 127673 kitakachofanyika tarehe **11/3/2024** ofisini kwa mfilisi saa 4:30 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

Mfilisi: **LINDA ALLAN MWAMBETE**

Amwani ya Mfilisi: **368 MSASANI ROAD MIKUMI HOUSE OYSTERBAY P.O BOX 9673 DAR ES SALAAM TANZANIA**

Tarehe ya kuchaguliwa: **20 SEPTEMBER 2023**

Amechaguliwa na: **WAMILIKI WA KAMPUNI**

**Sahihi** ............................................................ **Tarehe:** 9/02/2024

**Jina: LINDA ALLAN MWAMBETE**



Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, akijaribisha gari la kubebea wagonjwa, kabla ya kulikabidhi kwa uongozi wa Hospitali ya Wilaya ya Morogoro mwishoni mwa wiki. Gari hilo, limetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kufuatia ombi la mbunge huyo ili kusaidia huduma mbalimbali za afya. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Upasuaji wa kuongeza makalio Muhimbili wazua zogo bungeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MJADALA mkali umeibuka bungeni kuhusu upasuaji kurekebisha maumbile, ikiwamo kupunguza au kuongeza ukubwa wa makalio katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa (CCM), ndiye aliyeibua zogo bungeni jijini hapa juzi, alipotoa hoja kwamba MNH-Mloganzila imeanzisha huduma hiyo kinyume cha Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007.

Hospitali hiyo ilitangaza kuanza upasuaji huo wa mapambo 'Reconstructive Cosmetic Surgery' Oktoba 27, mwaka jana.

Wakati akichangia mjadala kuhusu Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi kwa Mwaka 2023, Mpina alihoji sababu za uongozi wa hospitali hiyo kutoa rukhsa ya jambo hilo wakati hakuna mahali kwenye Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007 imetoa baraka kuwa na huduma hiyo.

"Hakuna mahali kwenye Sera ya Afya yetu ya Mwaka 2007 imeruhusu jambo hili. Operesheni ya matibabu, operesheni kwa ajili ya kuongeza makalio; ni operesheni ya kimapambo (cosmetic surgery), si ya mtu ambaye ana changamoto yoyote ile ya afya.

"Kwahiyo, kwenye sera yetu jambo hili halipo. Kwanini Hospitali ya Mloganzila imeruhusu jambo hili kufanyika?" alihoji Mpina aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi katika uongozi wa Rais John Magufuli.

Baada ya Mpina kutoa kauli hiyo, Mbunge wa Gairo, Ahmed Shabiby, alisimama na kumpa taarifa Mpina, akisema hata kiuno kikikaa vibaya nayo ni changamoto ya kimatibabu.

"Kwahiyo, kukiweka kiuno vizuri, ni kusababisha binadamu atembee vizuri na aweze kuwa na umbo zuri," alisema Shabiby.

Hata hivyo, Mpina alikataa kupokea taarifa hiyo ya mbunge mwenzake, akisisitiza serikali imeanzisha huduma hiyo bila kibali cha Bunge wala hakuna sheria, kanuni na mwongozo wa utoaji huduma hiyo.

"Kwahiyo, wananchi wetu leo hii wakienda kupata matibabu makubwa kwenye huo upasuaji, hakuna sheria inayowaongoza katika kazi zao," Mpina alifafanua zaidi hoja yake.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisimama na kupinga vikali kilichoelezwa na Mbunge Mpina.

Naibu Waziri huyo ambaye kitaaluma ni daktari wa binadamu, alisema: "Mimi sina shida na mchango wa Mheshimiwa Mbunge (Mpina), ila tu nilitaka nimweleweshe kwamba kwenye tiba na kwenye tiba za kawaida; kwanza maana ya afya ni nini? Kuwa na afya si tu kutokuwapo magonjwa.

"Unaweza ukawa una afya, huna ugonjwa lakini una shida ya afya kwa sababu kisaikolojia hauko vizuri, wala kisosholojia hauko vizuri.

"Kwahiyo, sisi kiafya hatukuangalii wewe kwa maana ya ugonjwa. Binadamu si disease entity, ni partiality ya kimawazo, kiakili, kimwili na kila kitu."

Majibu hayo ya Naibu Waziri Mollel hayakumpendeza Mpina. Mbunge huyo akaendelea kusisitiza kuwa matibabu popote duniani yanaongozwa na sera ya nchi.

"Sera yetu ya nchi haijaziaccommodate (haijajumuisha) huduma zote. Huduma za kimapambo hazipo! Sasa huyu waziri anaongea nini?" Mbunge Mpina alihoji.

Swali hilo likamwibua Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyeinuka kwenye kiti na kusema wanaongozwa na tafsiri au miongozo ya Shirika la Afya Duniani (WHO), ambayo inaeleza afya ni ukamilifu wa binadamu kimwili, kiakili na kijamii na kutokuwapo magonjwa.

"Lakini, sera hii inatutaka tutoe huduma kwa kuzingatia mahitaji ya kila mtu. Watu wanakwenda India, Uturuki kutafuta huduma na wanakwenda kulipa dola. Wataalamu wetu wana uwezo, wamesoma, kwanini wasitoe huduma hizo ndani ya nchi?

"Hela (fedha) hizi hizi, ndio tunatibia hao wagonjwa wa msamaha. Hela hizi ndio tunatibia kinamama wajawazito. Hela hizi ndio tunatibia watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

"Kwahiyo, ni suala la vipaumbele. Watanzania wakaanze kupambana na ndege, wataalamu wapo (nchini) wamesoma. Usitegemee Muhimbili, akaenda kutibu malaria.

"Ile ni hospitali ya ubingwa na ubingwa bobezi. Leo imejielekeza kwenye 'reconstructive and cosmetic surgery' (upasuaji wa kuongeza na kurekebisha mwonekano) hakuna tatizo hapo," alisisitiza Waziri Ummy.

Hata hivyo, Waziri Ummy hakutoa maelezo kuhusu hoja ya Mbunge Mpina kama huduma hiyo mpya Muhimbili imezingatia Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007.

# Makonda anyooshewa kidole kauli kuhusu haki mahakamani

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA) na wadau wengine wa haki na utawala bora, wameitaka Mahakama kutoa tamko kuhusu kauli ya Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) - Itikadi na Uenezi, Paul Makonda dhidi ya chombo hicho.

Makonda aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa uongozi wa Rais John Magufuli, ananyooshewa kidole kutokana na kauli yake kwamba wananchi waache kukimbilia mahakamani, badala yake wapeleke kero zao kwa wateule wa Rais.

Akiwa katika ziara ya chama chake mikoa ya Nyanda za Juu Kusini mwanzoni mwa mwezi huu, Makonda aliwataka wananchi kupeleka kero zao kwa wateule wa Rais, akiwamo yeye kwa kile alichodai kukimbilia mahakamani huenda kukafanya wasipate haki.

Makonda alisema wananchi huenda wasipate haki katika chombo hicho kwa kuwa huko kuna aliowaita "wajanja wanaoweza kutumia mbinu kushinda kesi".

"Mimi mwenyewe hapa kuna mtu alinidhulumu nyumba, halafu wajanja wakaniambia 'nenda mahakamani'. Nikapiga mahesabu mahakamani kwa jinsi huyu mtu alivyo na hela (fedha) nitatoboa?

"Nikasema Mungu atanipa mlango na Mungu amenipa. Kwahiyo, msikimbilie wapi... msikimbilie mahakamani, wale wajanja wana mbinu zao.

"Wanasheria kazi yao ni kumtetea mteja wao, hata awe ameua, (wakili) jukumu lake amtetee mteja wake na yeye ni lazima aoneshe ni wakili bingwa. Kwahiyo, ukiwa huna wakili bora, unaweza kupoteza haki yako.

"Ndiyo maana unashangaa watu wengi maskini kesi zao zina miaka 10, miaka 20, miaka 15 inapigwa tarehe, inatubidi tubanane huku huku kwa wateule wa Dk. Samia Suluhu Hassan," Makonda alisema.

BAVICHA katika taarifa yao ya jana kwa vyombo vya habari, wanashauri uongozi wa Mahakama kutoa kauli ili kurejesha imani ya wananchi kwa muhimili huo kuhusu utoaji haki bila kujali hali ya kipato aliyonayo mtu wala hadhi yake katika jamii.

BAVICHA kupitia taarifa yake hiyo iliyotiwa saini na Apolinary Boniface, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa baraza hilo, inasisitiza kuwa Taifa likikosa imani na mahakama, nchi haitatawalika.

"BAVICHA tunatoa wito kwa muhimili wa Mahakama kutoa kauli kuhusu alichokisema Mwenezi wa CCM, ni vyema umma ukajua kama ni kweli muhimili huo unatoa haki kwa wenye fedha tu na siyo kwa wananchi wa hali zote.

"Mahakama isipotoa kauli ya kukemea na kukanusha kauli hiyo ya Makonda, itawaaminisha wananchi kujichukulia uamuzi mkononi kutokana na kukosa imani kwa muhimili huo kama utawatendea haki," BAVICHA inaeleza katika taarifa yake hiyo.

Mwandishi wa Habari Mkongwe, Ndimara Tegambwage pia ameshauri Mahakama na Bunge kutoa kauli kuhusu suala hilo ili kutokufifisha misingi ya haki na utawala bora na kutegemea wateule wachache kupata haki zao.

"Mahakama ina cha kusema hapa juu ya kauli ya CCM kuwa wananchi wasiende mahakamani, Bunge lisimame na kusema inatosha na kukemea yule anayelenga kuleta utawala wa mfukoni usio wa sheria na wa kidhalimu.

"Chama cha Wanasheria (TLS), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), asasi hai za kijamii, vyombo vya habari na wote wenye mapenzi mema kwa Tanzania, wana kitu cha kusema. Wakiseme wapinge 'ushetani' huu.

"Ninatambua vyama vya siasa ni asasi za kijamii, tuone na tusikie kauli zao kwa hili... Mkoa wapi magwiji wa sheria – binafsi na kampuni na wapigania uhuru na haki kazini, mitaani na vyuoni? Mnakaa kimya ili iweje?" Ndimara alihoji.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe alisema jana kuwa kauli ya Makonda inaweza kuwa na tafsiri tofauti kuhusu mfumo wa utoaji haki wa Mahakama kwa watanzania hasa kwa wale wasiokuwa na fedha.

Alisema kuwa mtu anaweza kupata haki kwa kutumia njia zisizokuwa rasmi kuliko zile zilizo rasmi.

"Kauli ya Makonda inaweza kuwa na tafsiri tofauti. Moja ikiwa ni kutoarifu umma wa watanzania kuwa mfumo wa Mahakama si salama katika kupata haki, hususani kwa watu wasiokuwa na fedha na pili tafsiri kuwa unaweza kupata haki kupitia njia zingine zisizokuwa rasmi," alisema.

# TEC yatoa ujumbe wa Kwaresma ukibeba hoja nzito kisiasa, familia

**Na Restuta James**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) limetoa ujumbe wa Kwaresma wenye sura nne ndani ya kurasa 39, ambao pamoja na mambo mengine, unazungumzia imani, maadili, siasa, utamaduni, tunu za kiutu, uchumi na mazingira.

Ujumbe huo wenye kichwa 'Nitawezaje Kuelewa Mtu Asiponiongoza', umetiwa saini na maaskofu 38, akiwamo Rais wa TEC, Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga wa Jimbo la Mbeya na Mwadhama Protase Kardinali Rugambwa wa Tabora.

Sura ya kwanza ya ujumbe huo inazungumzia umuhimu wa neno la Mungu, huku ikitoa mfano wa mahangaiko ya Towashi anayetajwa kama mtumishi wa aliyekuwa Malkia wa Ethiopia, ikiweka msingi wa umuhimu wa mtu kuongozwa ili kufikia wongofu.

Sura ya pili ikiwa na vipengele vitatu, inaweka msingi wa wongofu hasa mahangaiko, hitaji la kuongozwa, ujasiri na unyenyekevu.

"Yote mawili, kuongoza na kuongozwa, yanahitaji ujasiri na unyenyekevu... kiongozi yeyote anapaswa kuwa jasiri na aweze kukabili tatizo. Aidha, awe na unyenyekevu wa kufanya yote kwa upendo na hivyo kukubalika na yule anayemwongoza," inaeleza sehemu ya ujumbe huo.

Ujumbe huo unakumbusha wajibu wa familia na kanisa katika eneo la malezi, ili kuandaa viongozi wazuri wenye sifa stahiki.

"Tunaposhindwa kupata viongozi wenye sifa nini kinatokea? Viongozi watatengenezwa ili wawe na sifa ya viongozi ingawa kimsingi hawana sifa hizo. Ndiyo maana tunaona makundi yakipita hapa na pale wakitumia nguvu nyingi, wakati mwingine hata za fedha ili tu yule wanayemfikiria apite," unasema.

Ujumbe umewaelekeza viongozi kufuatilia watu wao na kujua wanaweza nini na hawawezi nini.

"Wawe na huruma kwa watu wao na wawe tayari kuwasaidia kadri wawezavyo. Waongozwa, nao wawe wanyenyekevu wa kusikia na kutii sauti ya viongozi wao, wawe na ujasiri wa kuuliza, kukubali kukosolewa, kusahihishwa na kurekebishwa," unafafanua.

Ujumbe huo unataka watu wajitathmini kwa Neno la Mungu ili kutoa uamuzi wa kubadilisha mtindo wa maisha kwa kuacha maelekeo ya dhambi kwenda yale yanayomfurahisha Mungu.

Kuhusu imani, siasa, maadili, tunu za kiutu na uchumi, ujumbe huo unafafanua athari za kutofahamu neno la Mungu kunavyoharibu maeneo hayo.

"Kutokana na kutokuwa na ufahamu wa kina wa Maandiko Matakatifu, wale wenye mamlaka wakati mwingine wanajikuta wanafumbia macho maovu mengi yenye athari kubwa kwa familia zetu na jamii yetu. Kinachoshuhudiwa kwa sasa ni mmomonyoko mkubwa wa maadili kwa rika zote," unafafanua.

Kwenye uchumi, ujumbe huo unaeleza kuwa watu wote wameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu na hivyo kuwafanya wote wawe sawa kiutu.

"Ubinafsi unaojidhihirisha katika vitendo kama vile wizi, ukwepaji kulipa kodi halali, ulipishaji wa kodi zisizo halali na kwa manufaa binafsi, rushwa, ufisadi na magendo, vinaashiria kutoongozwa na Neno la Mungu.

"Tofauti kubwa baina ya walio nacho na wasio nacho au matajiri wa kupindukia na maskini wa kupindukia ni matokeo yake. Neno la Mungu lituongoze ili tuwe watu wa kiasi, haki na upendo.

"Kisiasa kutojua vizuri Neno la Mungu kwa wakati mwingine kumewapelekea watu (wanasiasa), kutafuta vyeo kwa njia ya rushwa, wizi wa kura na hata mahali pengine ya kutoa uhai wa watu wengine.

"Katika nchi nyingi za Kiafrika hili limekuwa "donda-ndugu" ambalo matokeo yake ni migogoro ya kivita na mapambano ya kiitikadi. Hii pia inatokana na tamaa mbaya za kisiasa ambazo mwelekeo wake ni kulinda maslahi binafsi na ulafi wa madaraka," ujumbe wa Kwaresma unaeleza.

Inaelezwa katika ujumbe huo kuwa hali hiyo inachochea mipasuko ya kisiasa ndani ya jamii kwa sababu ya kikundi kimoja kujiona bora kuliko kingine na wakati mwingine kujiona kiko juu ya sheria za nchi.

Sura ya nne ya ujumbe huo inapendekeza kuwa watu wasome Neno la Mungu kila siku ili kukua kiimani.

Kiuchumi, ujumbe unaeleza kuwa uchumi wa taifa unategemea rasilimali za nchi zitumike kuwanufaisha wengi.

Sehemu ya ujumbe huo inasema: "Hili linaweza tu kufanyika kwa kuwa na hofu ya Mungu aliyetupatia rasilimali zote kama zawadi kwetu.

"Ujumbe wetu wa Kwaresima wa mwaka huu unahimiza na kuwaalika wale wanaotumia nafasi zao, uelewa wao na mamlaka yao kujilimbikizia na kumiliki rasilimali ambazo Mungu amezitoa kwa ajili ya watu wote badala yake wao wanazitumia kwa manufaa yao na familia zao.

"Shibe yao ya leo inayowaumiza walio wengi; na wao wenyewe inawafungulia mlango wa mateso wa maisha ya baadaye." Ujumbe huo pia unakumbusha waraka wa Kwaresima uliotolewa na TEC mwaka 2014, ambao ulikumbusha wajibu wa wenye mamlaka kuhakikisha wananufaisha wengi.

"Kisiasa kanisa linaamini kuwa kiongozi yeyote (halali) anatoka kwa Mungu, lakini namna ya kuongoza kwa uadilifu katika wajibu wake inategemea uwezo wake na hofu ya Mungu aliyonayo.

"Siasa ni sauti ya watu kwa ajili ya watu wenyewe; bila shaka hawawezi kuitoa sauti ambayo wao wenyewe hawana. Ikiwa siasa inafikiriwa na kuchukuliwa katika maana ya "siasa ni viongozi", basi tutaendelea kuyashuhudia mengi yasiyo halali, haki wala uadilifu," unaonya.

Ujumbe huo pia umewataka viongozi wa ngazi zote wawe wakweli, wanyofu na mwenye kuwajibika kwa kuendeleza mema na kukemea yaliyo maovu na kuyasahihisha.

Kwaresma ni kipindi ambacho Wakristo wanakumbuka mateso, kifo na ufufuko wa Yesu Kristo kwa ajili ya kuukomboa ulimwengu.



Wanawake wakiwa kwenye foleni ya kuchota maji katika Mtaa wa Mdote, Kata ya Majengo, wilayani Muheza mkoani Tanga jana, baada maji kuwa adimu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mawaziri wawili wa JK wafariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

MAWAZIRI wawili waliohudumu katika serikali ya awamu ya nne, Balozi Diodoros Kamala na Dk. Ibrahim Msabaha, wamefariki dunia juzi na jana, mtawalia, familia zao zimethibitisha.

Balozi Kamala alikuwa Mbunge wa Nkenge (CCM) kwa vipindi vitatu (2000-2010 na 2015-2020), Naibu Waziri wa Wizara ya Afrika Mashariki (2006-2008 na Waziri kamili 2008-2010) kisha Balozi wa Tanzania Ubelgiji na Uholanzi (2011 hadi 2015). Familia ya Kamala kupitia dada yake, Ritha Kamala imethibitisha kifo cha mwanadiplomasia huyo aliyezaliwa Novemba 26, 1968.

Kwa upande wa Dk. Msabaha, familia imeeleza kuwa alifariki dunia mapema jana alipokuwa anapelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kupata matibabu.

Dk. Msabaha aliwahi kuwa Mbunge wa Kibaha (CCM) na Waziri wa Nishati na Madini kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Alijiuzulu uwaziri mwaka 2008 baada ya Kamati Teule ya Bunge iliyochunguza kashfa ya Richmond kumweka matatani kuhusu uhalali wa kampuni hiyo ya Marekani kupewa zabuni ya kufua umeme wa dharura.

Sababu za Dk. Msabaha kujiuzulu akiwa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kwa kuwa alikuwa Waziri wa Nishati na Madini wakati mkataba wa kufua megawati 100 za umeme wa dharura unatiwa saini kati ya serikali na kampuni ya Richmond.

Dk. Msabaha pia aliwahi kuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) katika Idara ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Anwani ya Simu: "Uvuvi"
Simu Nambari: +255 (026) 2322612
Nukushi: +255 (026) 2322613
Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz
Tovuti: http://www.mifugouvuvi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2847,
**40487 DODOMA**

**14 Februari, 2024**

## TAARIFA KWA UMMA

### USAJILI WA VYOMBO VYA UVUVI NA UKATAJI WA LESENI ZA VYOMBO VYA UVUVI KWA MWAKA 2024

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inapenda kuwatangazia wananchi wote wanaojishughulisha na uvuvi kwamba, msimu wa kukata leseni za vyombo vya uvuvi umeanza tangu Januari 1, 2024. Kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009; Kanuni Na. 3 (1-4), Kanuni 4 (1-6) na Kanuni 13 (1) chombo chochote kinachojihusisha na shughuli za uvuvi ni lazima kiwe kimesajiliwa na kukatiwa leseni.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, Kanuni 7(3) na (4), Chombo kilichopatiwa hati ya usajili na kupewa namba, inatakiwa namba hiyo iandikwe katika ubavu pande zote mbili za chombo. Kanuni ya 7 (1-5) na Jedwali la 3 inatoa mwongozo wa uandishi wa namba za usajili zinavyotakiwa kuwekwa katika chombo.

Zoezi la usajili na utoaji wa leseni za uvuvi litaisha tarehe 31 Machi, 2024, baada ya hapo wamiliki wa vyombo vya uvuvi watakaobainika kuwa hawajasajili vyombo vyao wala kukata leseni za uvuvi watachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kulipa faini kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi. Taratibu za usajili wa vyombo na Leseni za uvuvi zinapatikana katika tovuti ya Wizara **(https://www.mifugouvuvi.go.tz)**, Ofisi za Kanda za Wizara na Halmashauri zote zenye shughuli uvuvi nchini.

Imetolewa na;

**Prof. Riziki S. Shemdoe**
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Katika hili TCRA inastahili kongole, kazi isonge mbele

**UTAPELI** au wizi wa mtandaoni unaofanywa na watu mbalimbali, umekuwa ukishamiri siku hadi siku huku maelfu ya Watanzania wakilalamika kuibiwa fedha. Watu hao wanaotumia mitandao ya simu kufanikisha azma hiyo, wamekuwa ama wakiwapigia watu kwamba kuna fursa za kibiashara, kuwa wametumiwa fedha kimakosa kupitia namba zao au kuwataka wafanye miamala maarufu kama 'lipa kwa namba hii'.

Sambamba na mbinu hiyo, baadhi ya matapeli hao wamekuwa wakiwapigia watu hususan wazazi wa watoto wanaosoma katika shule za bweni wakijifanya walimu kwamba ama wamelazwa hospitalini, hivyo watume fedha za matibabu kupitia namba wanazowaelekeza. Kwa mfumo huo, baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakiamini kuwa watoto wamepata tatizo, hivyo kutuma fedha na wanapogundua kuwa si kweli, wanajikuta tayari wameshaibiwa fedha.

Kwa ujumla, vitendo hivyo vilikuwa kero miongoni mwa Watanzania hasa wale ambao wamekuwa wakifanya hivyo kwa kudhani kuwa wamewalipa fedha hizo watu waliokuwa wakiwadai au kulipa kwa ajili ya michango.

Kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo, watu wengi wamekuwa wakizitupia lawama kampuni za mawasiliano ya simu na wakati mwingine wakishuku kwamba baadhi ya wafanyakazi wao wanashirikiana na matapeli hao kuwaibia fedha wananchi.

Lawama zingine zimekuwa zikielekezwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwamba inashindwa kuzidhibiti kampuni za simu na watu wanaojihusisha na mitandao hiyo ya kihalifu au wizi wa mtandaoni. Hatua hiyo kwa kiasi kikubwa iliiamisha TCRA kutoka usingizini na kuanza kuchukua hatua ikiwamo kuzifungia laini zinazotumika katika kufanya uhalifu huo.

Katika kuchukua hatua hizo, TCRA juzi ilitangaza kuzifungia laini 21,788 za simu zilizohusika na utapeli huo katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Mkurugenzi Mkuu wa TCRA alisema laini hizo zimefungiwa kutokana na kubainika kufanya matukio ya utapeli na wizi wa mtandaoni.

Ripoti hiyo ya hali ya mawasiliano imebainisha kwamba kampeni hiyo ya kuzifungia laini hizo imeonekana kuzaa matunda kutokana na kupungua kwa matukio kama hayo kwa kuwa katika kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka jana, laini 23,328 zilifungiwa. Juhudi hizo zinaonyesha kuwa kumekuwa na matokeo chanya kwa kuwa takwimu zinaonyesha matukio hayo yamepungua kwa asilimia 6.6, jambo ambalo ni la kujivunia.


Mafanikio hayo, kwa mujibu wa TCRA, yanatokana na ushirikiano baina ya kampuni zinazotoa huduma ya mawasiliano ya simu na vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na mwamko wa wananchi katika kuripoti namba zinazoshukiwa kuwa zinajihusisha na utapeli huo.

Jitihada zilizofanywa katika kukomesha vitendo hivyo zimeonyesha wazi kwamba kuna mafanikio katika vita hivyo ambavyo awali vilionekana sawa na mfupa uliomshinda fisi kutokana na kushamiri na kudhaniwa hakuna hatua zinazochukuliwa. Ni wazi kwamba kama mafanikio yalivyoonekana katika kipindi kifupi, wahusika hao watabanwa ipasavyo kama ushirikiano uliopo hivi sasa.

Pamoja na mafanikio hayo, jitihada zaidi zinatakiwa kufanyika zaidi kuanzia kwenye usajili wa laini kwa kuwa imebainika kwamba baadhi ya laini zinazotumika hazina majina rasmi ya wahusika. Kwa mantiki hiyo, kinachotakiwa kufanyika ni pamoja na kudhibiti usajili wa simu kwa kuwa hivi sasa kila mahali kazi hiyo inafanyika, hivyo watu wote wanaohusika ni muhimu wawe na leseni kutoka TCRA.

Kwa hiyo kama kuna upungufu katika sheria ya mawasiliano, ni vyema serikali ikaanzisha mchakato wa kuifanyia mabadiliko ili kusimamia ipasavyo suala zima la umiliki wa laini za simu kuanzia ngazi ya kusajili laini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Lowassa ameacha somo ni uvumilivu wa kisiasa

Na Sabato Kasika

**MWAKA** 2008 Edward Lowassa wakati huo akiwa Waziri Mkuu, alijiuzulu nafasi hiyo kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kashfa ya kutuhumiwa kuhusika kuibeba kampuni ya Richmond, ambayo licha ya kupewa jukumu la kuzalisha umeme, haikufanya hivyo na nchi ikazidi kubaki gizani.

Wakati akitangaza kujiuzulu, alilalamika kutopewa nafasi ya kujieleza kuhusu tuhuma hizo, na kuhitimisha kuwa shida ni huu uwaziri mkuu, hivyo akaamua kuacha nafasi hiyo.

Baada ya uamuzi wake huo, baadhi ya wanasiasa wakiwamo wa kutoka CCM na upinzani, walimpachika kila aina ya majina ya kashfa na kurushiwa maneno mengi kuhusu tuhuma hizo, hata Richmond ikitafsiriwa kuwa ni kampuni yake binafsi iitwayo 'Rich Monduli.'

Lakini mwenyewe hakuthubutu kufungua mdomo wake kuwajibu au kulumbana nao, badala yake alikaa kimya na kuendelea na shughuli zake zikiwamo za kisiasa wakati huo akiwa mbunge wa Monduli.

Lowassa ambaye sasa ni marehemu, mwaka 2015 alikuwa miongoni msururu mrefu wa makada wa CCM walioomba ridhaa ya chama hicho, kumpitisha kuwania urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huo.

Hata hivyo, alihama chama hicho na kwenda CHADEMA dakika za mwisho, baada ya kuona amekatwa katika mchakato wa kumpata mgombea wa chama hicho wa kuchuana na wapinzani.

Kuondoka kwake ilikuwa ni kama kufungulia upya matusi, kejeli, kashfa na kila neno baya dhidi yake kutoka kwa baadhi ya makada wa CCM, lakini kama kawaida yake hakufungua mdomo kuwajibu.

Badala yake aliendelea na kampeni za kuwania urais kupitia chama kipya alichohamia na kuleta ushindani mkali katika kampeni za uchaguzi kwenye mikoa mbalimbali alikokuwa akipita.

Huku kila aina ya vijembe na kejeli na mambo mengine vikiendelea dhidi yake katika kampeni hizo, Lowassa aliendelea kumwaga sera za chama kipya na mikakati yake ya ambavyo angeongoza nchi.

Baadaye mwanasiasa huyo alirudi CCM hadi alipopatwa na mauti, lakini kama alivyohama CCM kwenda upinzani, ndivyo pia alirudi CCM bila kuthubutu kupanua mdomo wake kutukana na kukashifu kule alikotoka.

Tangu aliporudi CCM, aliendelea kuwa kimya. Huyo ndiye Lowassa mwenyewe ambaye alikuwa na uwezo wa kuvumilia siasa za majitaka alizokumbana nazo akiwa CCM na hata nje ya chama hicho.

Ninadhani yapo mengi ambayo wanasiasa wanaweza kujifunza kwake kupitia uvumilivu wake licha ya kutukanwa kiasi kile,lakini hakuthubutu kujibu neno au kuanzisha malumbano, badala yake alinyamaza kimya.

Mwanasiasa huyo alijua umuhimu wa kutotengeneza maadui, badala yake alijitahidi kuwafanya marafiki wale katika siasa walikuwa wakimchukia na kuwaacha wamkosoe au wamseme watakavyo.

Alikubali kukosolewa, kusemwa vibaya hata kwa yale ambayo hakutenda. Mfumo wake huo wa maisha katika siasa za Tanzania, atakuwa ameawachia wanasiasa jambo la kujifunza kuvumiliana.

Huyo ndiye Lowassa ambaye alikuwa tayari kusemwa vibaya, lakini pia kukosolewa, kwani alitambua kwamba kukosolewa ni jambo la kawaida ambalo linampa mtu nafasi ya kujisahihisha pale alipokosea.

Lowassa ametangulia, lakini amewaachia wanasiasa somo la uvumulivu wa kisiasa, kwamba wanaweza kutofautiana,lakini wakavumiliana kwa kuwa wote wanajenga nyumba moja ambayo ni Tanzania.

Mwili wake unatarajiwa kuagwa leo kwenye ibada itakayofanyika katika Kanisa la Azania Front jijini Dar es Salaam, kisha kesho utasafirishwa kwenda jijini Arusha na kuagwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na familia ya Lowassa, siku ya Ijumaa ibada ya kuaga mwili wake itafanyika Monduli na kufuatiwa na maziko yatakayofanyika Monduli Jumamosi.

# CHADEMA yalia kutopewa nafasi

**Na Pilly Kigome**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimelalamika kunyimwa nafasi ya kutoa salamu za pole katika hafla ya kuuaga mwili wa Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, ameelekeza malalamiko kwa Itifaki ya Kamati ya Maandalizi kuwa haikuwapa nafasi ya kufanya hivyo kama vyama vingine vilivyopewa.

Akizungumza jana katika viwanja vya Karemjee, ambako hafla ya kuuaga mwili wa Lowassa ilifanyika, alisema haikuwa sawa kutopewa nafasi ya kuzungumza kwa kuwa Lowassa alitumikia chama hicho kwa kipindi kirefu na alikuwa mwanaharakati wa kutaka mabadiliko mengi akiwa katika chama hicho.

Mnyika alisema Lowassa alihamia katika chama hicho mwaka 2015 akitokea Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya kukatwa kwenye kinyang'anyiro cha urais na kuteuliwa kugombea urais kupitia Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA).

"Imenishangaza kwa kunyimwa nafasi hiyo kwani mimi kama katibu mkuu niko hapa ningeweza kukisemea chama na wanachama wa CHADEMA kwa ujumla kwa mazuri yake aliyoyafanya akiwa na chama chetu," alisema Mnyika.

Alisema pamoja na mambo mengine kiongozi huyo alikuwa muumini wa mabadiliko ya mfumo wa utawala kwa kupitia katiba mpya, hivyo namna nzuri ya kumuenzi ni kufanya marekebisho ya katiba ili kuwe na uchaguzi huru na wa haki.

"Ndiyo maana alipopeperusha bendera ya CHADEMA. Kipaumbele namba moja ni kuwa na katiba mpya, hivyo amefariki (dunia) bado katiba mpya haijapatikana, hivyo ni muhimu mchakato huo uendelee," alisema Mnyika.

Aidha, alisema Lowassa aliingia katika chama akiwa na sera nzuri ambazo alizisemea kwa lugha yake ikiwamo uchumi imara na shirikishi unaogusa maisha ya watu kwa kuleta unafuu.

**VYAMA VYA SIASA**

Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa Tanzania, Juma Khatibu, aliwasihi wananchi wawe wastahimilivu katika kipindi hiki kigumu kilicholikumba Tanzania.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Anamringi Macha, alisema kila mmoja kwa nafasi yake arejee mema ya kiongozi huyo ili kulijenga taifa.

Alisema chama hicho kimejifunza mengi kutoka kwake na watayarejea kwa ajili ya kuijenga nchi, chama na siasa ya nchi.

**MAHAKAMA YATOA NENO**

Akizungumza kwa niaba ya Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, Jaji Jacob Mwambwgele, alisema Mahakama ya Tanzania inamfahamu Lowassa kama mwanasiasa mwenye moyo wa uvumilivu, mwenye ngozi ngumu ya kisiasa.

Jaji Mwambegele alisema kiongozi huyo alikuwa akiuishi msemo wa kuwa 'ukimya ni dhahabu' na mahakama hiyo imelichukua hilo kama funzo katika maisha hao ya duniani.

Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba alisema kiongozi huyo alikuwa mwenye kiu ya kupenda matokeo zaidi kuliko maneno na pia si mchoyo wa mawazo.

"Nimepoteza rafiki, nimepoteza kiongozi nakumbuka alinijenga katika mambo mengi hasa bungeni alikuwa ananielekeza mambo mengi na kunipa mwongozo," alisema Nchemba.

# Serikali yapeleka kicheko kwa wazabuni ikiwalipa Tril. 1.03/-

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imesema imelipa jumla ya Sh. trilioni 1.03 za madeni ya wazabuni yaliyohakikiwa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (IAG) na kukidhi vigezo.

Malipo hayo ni sawa na asilimia 73 ya madeni yote yenye jumla ya Sh. trilioni 1.41.

Bungeni jijini Dodoma juzi, Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alibainisha hayo alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Ritha Kabati aliyetaka kufahamu idadi ya wazabuni waliolipwa na serikali.

Wazabuni hao ni wanaozidai taasisi mbalimbali nchini, mbunge huyo pia akihoji kiasi cha fedha kilicholipwa na serikali kwa kundi hilo.

Naibu Waziri Chande alisema idadi ya wazabuni waliolipwa ni 8,830 ambao walikuwa wakidai taasisi mbalimbali za serikali.

Alisema ulipaji huo ni hatua ya serikali katika kuchochea uchumi na kukuza sekta binafsi. Alisema serikali inaendelea kuwalipa wazabuni kwa kadri fedha zitakavyopatikana na pia ulipaji ni lazima ufuate taratibu kwa kuwa suala la zabuni hutolewa kwa mkataba na ni suala la kisheria.

## KABWELA Na Fadhili Mohammed





GARDAWORLD

## INVITATION FOR PRE-QUALIFICATION OF SUPPLIERS GW/2024-2026/PQ/01

**GARDAWORLD TANZANIA LIMITED** is the leading security provider in Tanzania, GW has been providing security services to the Private and Commercial sectors in Tanzania since 1999.This has been predominantly in the mining, agricultural, and industrial, commercial, and Residential security market throughout Tanzania.

The company boasts of being the market leader in Tanzania providing a full range of security services, ranging from man guarding security dogs and robust electronic security solutions.

GW now invites suitably qualified and competent bidders to submit sealed prequalification bid for the supply of various goods, services and works for the Financial Year 2024-2026. In one or more of the categories appearing below. The objective of the prequalification is to identify competent individual /firms /companies that will be called upon from time to time to quote / tender for supply of goods, services and works during the financial year 2024/2026

| | CATEGORY DESCRIPTION |
|---|---|
| | **SUPPLY OF GOODS** |
| GW 2024/01 | Supply and delivery of general office stationery and computer consumables |
| GW 2024/02 | Design and printing of promotional, communication and corporate branded materials |
| GW 2024/03 | Supply and delivery of tailored staff uniforms and footwears |
| GW 2024/04 | Supply and delivery of Protective clothing and equipment |
| GW 2024/05 | Supply and delivery of general alarms, CCTV and Access Control devices and biometric equipment |
| GW 2024/06 | Supply and delivery of ICT equipment, computers, Laptops, Tablets Computer bags ,servers and related accessories |
| GW 2024/07 | Supply and servicing of VHF Radios, Batteries, chargers, antennas, repeaters etc. |
| GW 2024/08 | Supply of motor vehicle, spare parts, tyres, tubes, batteries and accessories (majorly,Toyota single and double cabs ets ) |
| GW 2024/09 | Supply of office furniture, furnishes, assorted fixtures and fittings |
| GW 2024/10 | Supply, servicing, and maintenance of air condition equipment |
| GW 2024/11 | Supply and delivery of dog feeds and dog handling equipment |
| GW 2024/12 | Supply of Fuels and Lubricants |
| GW 2024/13 | Supply, installation and maintenance of generators |
| GW 2024/14 | Supply, delivery, and maintenance of firefighting equipment |
| GW 2024/15 | Supply and delivery hardware, Electricals, and construction materials. |
| GW 2024/16 | Supply of security seals and accessories |
| GW 2024/17 | Supply of office kitchen supplies (sugar, milk, coffee, bottled drinking water, water dispensers, beverages etc.) |
| GW 2024/18 | Supply and delivery of general office toiletries , cleaning detergents ,cleaning accessories and equipments |
| | |
| | **PROVISION OF SERVICES** |
| GW 2024/19 | Motor vehicle's servicing, maintenance & repairs |
| GW 2024/20 | Motorcycle's servicing, maintenance & repairs |
| GW 2024/21 | Provision of car hire (short and long term) and leasing services |
| GW 2024/22 | Provision of multifunctional printers leasing services |
| GW 2024/23 | Provision of Clearing and Forwarding services |
| GW 2024/24 | Provision of corporate branding services e.g., branding of vehicles, installation of vinyl stickers for walls,window markings,exteroir led signage etc |
| GW 2024/25 | Provision of travel and air ticketing services |
| GW 2024/26 | Provision of dog veterinary services, health medicines and supplies (anti-tick, de-wormers etc.) |
| GW 2024/27 | Provision of fumigation services (pest control) |
| GW 2024/28 | Provision of recycling services (recycling of old used Askari uniforms and boots) |
| GW 2024/29 | Provision of motor vehicle valuation services |
| GW 2024/30 | Provision of catering services |
| | **PROVISION OF WORKS** |
| GW 2024/31 | Provision of minor construction services including tile works, repainting (interior and exterior) and renovation services |

1. The Prequalification document with details can be obtained during working hours from GardaWorld Offices, DAR ES SALAAM, MWANZA, and ARUSHA. A complete set of Prequalification document(s) shall be purchased by interested applicant on submission of a written application letter to the address given under paragraph below and upon payment of a nonrefundable fee of TZS 50,000/- per category applied. Payment should be made at NCBA Bank A/C 103895100026 Kenya Kazi Security (T) Ltd. Please note that if you intend to provide multiple goods / services, a separate prequalification of suppliers document must be submitted for each category.

2. All existing suppliers are advised to participate alongside prospective suppliers in order to be evaluated and considered. Please note that Prequalification is not a guarantee for business opportunity, bidders will be invited to submit their quotations on need basis based on the opportunities available.

3. GW reserves the right to accept or reject any applicant wholly or in part and is not bound to accept the lowest offer. Prospective bidders are hereby notified that canvassing of any kind will lead to automatic disqualification. GW may plan to visit supplier premises to verify information contained in the bid documents and obtain assurance of the vendor's capacity to deliver.

4 .Pre-qualification in plain sealed envelopes clearly marked "Pre- qualification of Supplier for FY 2024/2025" and indicating the category number applied for on the envelope should be dropped at GW office (upon signing of register as evidence of submission) and addressed to:

**Procurement Committee**
**GardaWorld Tanzania Ltd**
**PLT 16, Lucy Lameck Street**
**P.O. Box 12747**
**DAR ES SALAAM**

**Branch Manager**
**GardaWorld Tanzania Ltd**
**PLT 40, Nassa Rd, Capri point**
**P.O. Box 2076**
**MWANZA**

**General Manager**
**GardaWorld Tanzania Ltd**
**PLT 11 Simeon Rd, Kijenge Area**
**P.O. Box 10675**
**ARUSHA**

**The closing date for the submission of applications for Prequalification of Suppliers is Friday, 1st March, 2024 5.00 PM**

# Serikali yachunguza mitihani ya Shule ya Mafunzo ya Sheria

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imesema serikali imeitaarifu rasmi nia yake ya kuwasilisha bungeni marekebisho ya Sheria ya Shule ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo (LST).

Vilevile, imeeleza kuwa serikali kupitia Baraza la Elimu ya Sheria nchini, inafanya ukaguzi wa namna ya utungaji wa mitihani ya sheria kwa wanafunzi wa shule hiyo.

Marekebisho hayo ya LST yatakayofanyika, yanalenga kuwa na tija na manufaa mapana kwa taifa.

Hayo yamo katika taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati hiyo kwa kipindi cha kuanzia Februari 2023 hadi Januari 2024 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa jana na Mwenyekiti wake, Joseph Mhagama.

Mhagama, akizungumzia ufaulu wa wanafunzi wa kwenye shule hiyo, alisema serikali imeieleza kamati kuwa itapeleka bungeni marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Sura ya 425.

Alisema kuwa kupitia ukaguzi wa serikali unaoendelea, mapendekezo yanatolewa ili kufanya maboresho katika maeneo mbalimbali, ikiwamo miundombinu (majengo), idadi ya walimu wanaofundisha huko na sifa za walimu wanaohitajika kufundisha vyuo vikuu.

Maeneo mengine yanayokaguliwa ni maktaba za vyuo, kama kuna vitabu vya kutosha na vya kisasa, matumizi ya mtandao kwa wanafunzi katika kutafuta vitabu kwa ajili ya kujisomea, namna ya utungaji mitihani ya sheria kwa wanafunzi, ofisi za walimu vyuoni na mabweni ya wanafunzi.

Vilevile, alisema kuwa shule imeendelea kufanya maboresho mbalimbali katika kuinua ubora wa utoaji mafunzo ya sheria ikiwamo kuhuisha mtaala wake ili uendane na mahitaji ya soko.

Kwa mihula tofauti, matokeo ya mitihani ya uwakili yamekuwa mwiba kwa wahitimu wa shule hiyo ya sheria nchini.

Mwaka 2022, serikali iliunda kamati ya watu saba kuchunguza na kutafuta chanzo cha kufeli kwa wanafunzi wengi kwenye mitihani ya LST.

**DAWA ZA KULEVYA**

Katika hatua nyingine, Bunge limeazimia kuanzishwa rasmi Divisheni Maalum ya Kimahakama ya kushughulikia mashauri ya dawa za kulevya nchini baada ya kesi 64 pekee kati ya 1,158 kushughulikiwa katika kipindi tajwa.

Mhagama alisema ucheleweshwaji mashauri hayo unasababisha kupungua imani kwenye mfumo wa haki jinai nchini.

Alisema ucheleweshaji huo unachochea kuendelea biashara haramu na kuathiri juhudi za kupambana na dawa za kulevya.

Mbali na kuanzishwa kwa divisheni hiyo, Bunge limetaka watumishi na watendaji wa Mahakama kujengwa uwezo kwa kupatiwa mafunzo maalum ya uendeshaji mashauri yanayohusu dawa za kulevya kwenye mitandao (dark web).



Mbunge wa Makete, Festo Sanga (kulia), akijadiliana jambo na Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mpango kazi kutokomeza ukatili mbioni kukamilika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) awamu ya pili unatarajiwa kuzinduliwa Machi mwaka huu, moja ya vipaumbele vyake ni kudhibiti mimba za utotoni.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum, Mwanaidi Ali Khamis aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Janeth Mahawanga.

Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali kumaliza tatizo la mimba za utotoni kwa watoto wa kike.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mwanaidi alisema serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa inatekeleza afua mbalimbali kupitia mpango huo. "Pamoja na afua zinazotekelezwa katika mpango huo, serikali inaendelea kutekeleza mambo kufanyika kwa mapitio ya Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 ambayo imeongeza adhabu ya kifungo cha miaka 30 gerezani kwa atakayepatikana na hatia ya kumpa ujauzito mwanafunzi," alisema.

Alisema pia kuendelea kutoa elimu ya stadi za maisha kwa watoto kupitia madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto na kutoa elimu ya malezi na makuzi ya watoto kwa wazazi au walezi na jamii kupitia kampeni katika vyombo vya habari na majukwaa ya madhehebu ya dini.

"Serikali imepanga kuzindua kampeni ya usalama wa mtoto mtandaoni kwa ajili ya kuelimisha wazazi, walimu na watoto kuhusu athari za matumizi yasiyofaa ya mitandao ambayo pia yanachangia mimba za utotoni katika jamii," alisema.

# Waonywa kuwanyima safari watumishi wanaonyonyesha

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imekemea tabia ya baadhi ya waajiri katika utumishi wa umma kuwanyima safari wafanyakazi wanaonyonyesha kwa kigezo cha kutumia fedha nyingi za kujikimu.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alikemea tabia hiyo jana bungeni wakati anajibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatuma Toufiq.

Mbunge huyo alitaka tamko la serikali dhidi ya waajiri wanaowanyima safari wafanyakazi wanaonyonyesha kwa kigezo cha kutumia fedha nyingi za kujikimu.

Naibu Waziri Ridhiwani, akijibu swali hilo, alisema Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma (2008) 5.1 pamoja na Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma (2009) vinaelekeza watumishi wanaosafiri safari za kikazi, wakiwamo wanaonyonyesha kupewe posho ya kujikimu.

Alisema kwa kuzingatia maelezo hayo, serikali inaelekeza tena na kusisitiza kwa waajiri wote katika utumishi wa umma kuwa watumishi wa umma wahudumiwe kwa usawa na haki kwa kuzingatia sera na kanuni zilizopo.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji hatua zinazochukuliwa na serikali dhidi ya waajiri ambao hawawapi safari wanawake wanaonyonyesha.

Naibu Waziri Ridhiwani alisema hatua zimeendelea kuchukuliwa kwa waajiri wasiotekeleza majukumu yao ipasavyo ikiwamo ubaguzi wa safari kwa watumishi.

Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, katika swali lake la nyongeza, alisema tatizo linalokuta wanawake wanaonyonyesha, lipo pia kwa wenye watoto njiti.

"Wanatakiwa kukaa na watoto wao kwa muda mrefu, lakini waajiri wamekataa kuwalipa na kukataa kuwasaidia kulea watoto hao," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum, Santiel Kirumba alihoji kama serikali haioni haja kuwapa likizo ya uzazi zaidi ya siku 120 wanaojifungua watoto njiti ili kuwa na muda wa kutosha kuwatunza watoto hao.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Ridhiwani alisema kuwa katika utumishi wa umma, likizo ni miongoni mwa haki za watumishi wa umma ambazo wanastahili kupewa na waajiri wao kwa mujibu wa Kanuni H.12 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma (2009), ikisomwa pamoja na Kanuni ya 97 ya Kanuni za Utumishi wa Umma (2022).

Alisema suala la likizo kwa mtumishi aliyejifungua mtoto njiti halijaelezwa bayana kwenye Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma.



## Mwanafunzi darasa la kwanza anyongwa

**Na Vitus Audax**

MWANAFUNZI wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Magharibi Kambarage iliyoko mkoani Mara, Reuben (8), anadaiwa kuuawa kwa kunyongwa kisha mwili wake kutelekezwa katika eneo la shule hiyo.

Kwa mujibu wa wazazi wa mwanafunzi huyo, baada ya kuona kijana wao hafiki nyumbani ilhali muda wa masomo ulikuwa umeisha, ilibidi waende shuleni kuulizia kilichomsibu.

Walidai baada ya kufika shuleni, walibaini wanafunzi wote na walimu walikuwa wameshaondoka na shule imefungwa, lakini wakati wakizunguka katika maeneo ya karibu na shule, walibaini mwili wa kijana wao ukiwa katika moja ya vichaka karibu na shule hiyo.

Kufuatia tukio hilo Jeshi la Polisi mkoani humo limesema linawashikilia watu wawili ambao majina yao yamehifadhiwa kwa ajili ya mahojiano na uchunguzi ambao bado unaendelea.

Taarifa ya kukamatwa kwa watu hao ilitolewa juzi na Kamanda wa Polisi mkoani Mara, Salim Morcase na kueleza kuwa uchunguzi unaendelea na pindi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Katika hatua nyingine, Kamanda Morcase alisema jeshi hilo linawashikilia watu wawili ambao ni Paroko wa Kanisa Katoliki Parokia ya Bunda, Karoli Mganga pamoja na Mhasibu wa Parokia hiyo Gerald Mgendagenda kwa tuhuma za kujipatia zaidi ya Sh. milioni 800 kwa njia za udanganyifu.

Kamanda huyo alisema wawili hao wanadaiwa kughushi nyaraka kwa nyakati tofauti na kujipatia fedha hizo, mali ya parokia kinyume cha sheria na taratibu.

Alisema mbali na kughushi nyaraka hizo, wanatuhumiwa pia kughushi saini za watu mbalimbali zilizowawezesha kufanikisha malengo yao.

Vilevile, alitaja tukio la kukamatwa kwa Yusto Matange, mkazi wa Kijiji cha Majimoto, Wilaya ya Serengeti kwa tuhuma za kumkata viganja aliyekuwa mkewe, Kagembe George.

"Wawili hao walikuwa na shauri la mgogoro wa kifamilia mahakamani na hakimu alifikia uamuzi kuwa mume huyo hakuwa na haki ya kuendelea kuwa na mwanamke huyo kutokana na ukatili uliokithiri, lakini wakati wakiondoka, Matange aliingia kwenye shamba la mahindi na kutoka na panga na kuanza kumjeruhi huyo mwanamke ambaye anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando," alisema kamanda Morcase.

# 'Viongozi 'saccos' kuweni mabalozi wazuri wa uhifadhi'

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

VIONGOZI kutoka vikundi 10 vya kuweka na kukopa katika eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge, wameagizwa kuwa mabalozi wazuri wa uhifadhi, ili waendelee kunufaika na mitaji yenye masharti nafuu ya kuendesha vikundi vyao.

Vikundi hivyo vimepewa Sh.million 10 na Taasisi ya Chemchem Association inayofanya shughuli za uhifadhi katika eneo hilo ili wakopeshwe, kujikwamua na umasikini.

Katibu Tawala Msaidizi Mkoa Manyara, Faraja Ngerageza akizungumza wakati anafunga mafunzo kwa viongozi wa vikundi hivyo alisema viongozi wa vikoba ambao wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wanapaswa kuwa mabalozi wa wahifadhi.

Alisema taasisi ya chemchem imekuwa ikifadhili vikundi hivyo, ili vichangie kuendeleza uhifadhi, kupiga vita ujangili lakini pia kufanya shughuli za uzalishaji ili kujiongezea vipato.

Meneja wa miradi ya jamii ya chemchem, Napendaeli Wazoeli alisema taasisi hiyo imekuwa inawasaidia vikundi hivyo kukopeshana.

Alisema ili kuendana na sheria na kanuni za vikoba waliamua kusaidia wapatiwe elimu ili waweze waendane na sera ya mwaka 2019 ya serikali kuhusu vikoba inayowapa utambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Alisema licha ya vikundi kupatiwa mafunzo ya kanuni mpya, lakini pia vimepewa elimu ya kutunza fedha na wataalam wa Benki ya NMB, lakini pia vimepewa elimu ya uhifadhi wanyamapori.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Babati, Fadhila Nyambulapi alisema viongozi wa vikundi hivyo baada ya mafunzo wanatarajiwa kubadilika na kuendesha vikoba kisasa.



Mkuu wa mkoa wa Arusha, John Mongela (katikati), akikata utepe kuzindua mgahawa wa kitalii wa KFC, unaoendeshwa kampuni ya Dough Works Ltd, jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Dough Works, Vikram Desai. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Tanga kutoa chanjo ya surua, rubella watoto 318,108

**Na Hamida Kamalla,** TANGA

WATOTO zaidi ya 318,108 walio chini ya umri wa miaka mitano mkoani Tanga wanatarajiwa kupatiwa chanjo ya ugonjwa wa surua na rubella.

Akiongea na waandishi wa habari, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba alisema mkoa huo ni moja kati ya mikoa inayolengwa na kampeni hiyo ambayo itaanza rasmi Februari 15 hadi 18 ikiwa inalenga kutoa chanjo kwa watoto hao.

"Wizara ya Afya na TAMISEMI imepanga kuleta kampeni hii na tutaanza kampeni ya chanjo ya surua na rubela na Mkoa wa Tanga ukiwa mmoja wapo baada ya kuripotiwa kuwepo kwa ugonjwa wa surua katika wilaya tano," alisema.

Alisema kwamba magonjwa ya surua na rubela husababishwa na virusi ambavyo huenea kwa kasi sana kwa njia ya hewa, hasa pale mgonjwa anapokohoa au kupiga chafya. "Magonjwa haya huathiri watu wa rika zote lakini hasa kwa watoto walio chini ya miaka mitano, hivyo basi wananchi wote wazingatie ushauri wa wataalamu katika kuimarisha afya zetu na masuala ya usafi,

Kindamba alielezea dalili kuu za magonjwa hayo kuwa ni homa, mafua, kikohozi, macho kuwa mekundu na kutoa machozi lakini pia kutokwa na vipele vidogo katika paji la uso, nyuma ya masikio na hatimaye mwili mzima. Alisema magonjwa hayo yanasababisha madhara makubwa ikiwemo kutokwa na usaha masikioni ambapo yanaweza kusababisha matatizo ya kutosikia, lakini pia vidonda vya macho ambavyo husababisha kutoona au upofu, kubanwa mbavu na utapiamlo.

# Simanjiro wapitisha bajeti bil.39/- mwaka 2024/25

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wamepitisha bajeti ya Sh.bilioni 39 kwa ajili ya mapendekezo ya mpango wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025.

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Happynes Masatu akisoma bajeti hiyo alisema itakidhi kwenye sekta mbalimbali ikiwemo afya, elimu, kilimo na mifugo.

Masatu alisema bajeti hiyo imeandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa mpango wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2023/2024 na ilani ya uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2020/2025.

Alisema pia imelenga Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa miaka mitano, malengo ya maendeleo endelevu yam waka 2030 na Dira ya Taifa kwa mwaka 2025.


Aidha alisema katika sekta ya afya bajeti hiyo, itahakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya, katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kuhakikisha upatikanaji dawa na vifaa tiba. "Katika sekta ya elimu tutahakikisha tunaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwenye shule zote za msingi na sekondari kwa kujenga, kukarabati na kumalizia madarasa, mabwani, nyumba za walimu na vyoo," alisema Masatu. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Baraka Kanunga aliwasihi madiwani hao kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa watumishi wa halmashauri, katika utekelezaji wa bajeti hiyo.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema bajeti hiyo itawanufaisha wananchi wa eneo hilo kwani kata nyingi zimeguswa katika sekta tofauti.

Diwani wa Kata ya Ruvu Remit, Yohana Maitei alisema bajeti hii imekuwa na matumaini kwa upande wa sekta ya afya, elimu, kilimo na mifugo.

Diwani wa Kata ya Orkesumet, Sendeu Laizer alisema anatarajia bajeti hiyo itaboresha zaidi miundombinu ya elimu, kwani iliyopita ilifanikisha ujenzi wa madarasa mapya ya Shule ya Sekondari Simanjiro.

Diwani wa Kata ya Loiborsoit, Siria Baraka Kiduya alisema bajeti ya mwaka huu imeinufaisha kata yake, kwani itapata madarasa mawili, Shule Shikizi ya Songoyo na darasa moja katika Shule ya Msingi Losokonoi.





# RC aingilia kati ucheleweshaji wa ulipaji fidia kwa wananchi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri mkoani hapa kuhakikisha wanawalipa fidia wakazi waliotoa maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alitoa agizo hilo jana wakati akipokea mpango mkakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Kuna mambo ya kulipa fidia za viwanja na majengo ambayo tulichukua ya serikali kwa ajili ya matumizi ya umma na wenyewe wakati wa usikilizaji wa kero kila lalamiko mlikuwa mnakiri kutokuwalipa. hakikisheni mnawalipa fidia zao,"alisema Makalla.

Makalla pamoja na mambo mengine aliwaagiza viongozi na watendaji kusikiliza kero za wananchi na kuziwekea mikakati ya kuzitatua mara moja kwani wananchi wengi wamekua na shida mbalimbali za kimaisha, wanahitaji kusaidiwa.

Katika utatuzi wa migogoro na kero hizo Makalla aliagiza maamuzi yote yawekwe kwenye maandishi ili kurahisisha ufuatiliaji wa kero zilizosalia pamoja na kuweka kumbukumbu zao sawa.

Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Balandya Elikana aliitaka sekretarieti ya mkoa na menejimenti za halmashauri kuhakikisha katika upangaji wa bajeti wanazingatia msingi unaoleta tija kwa wananchi wanaowatumikia pamoja na kuwa na vyanzo vipya vya mapato ili kupanua wigo wa ukusanyaji.

Aidha, alisisitiza kuzingatia mipango na mikakati ya udhibiti wa fedha za umma kwa kuzingatia matumizi sahihi ya mashine za mifumo, pamoja na upelekaji wa fedha za mapato ya ndani kwenye miradi ya maendeleo kwa mujibu wa sheria.

Baadhi ya wakurugenzi kutoka katika halmashauri za mikoa walisema wameyapokea maelekezo hayo, huku wakiahidi kuwafuata wananchi kujua na kutatua kero zinazowasibu ikiwemo na ulipaji fidia pale inapobidi.

Mkurugenzi wa Halamshauri ya Magu, Fidelis Myovela: "Kwa Halmashauri ya Wilaya ya Magu tumetenga zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya ulipaji fidia wa baadhi ya maeneo ambayo tumeyachukua kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli na miradi ya maendeleo".



Msururu wa wafanyabiashara katika duka la msambazaji mkuu wa sukari Kanda ya Ziwa, Swami Shreeji 'V. H. Shah', wakisubiri kupata bidhaa hiyo, jijini Mwanza juzi, huku msambazaji huyo akidaiwa kuongeza bei ya sukari kutoka 70,000/- hadi 82,000/- kwa mfuko mmoja. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Wavamizi mgodi wa Barrick kikwazo utekelezaji shughuli za maendeleo

**Na Timothy Itembe,** MARA

UVAMIZI wa eneo la mgodi wa Barrick North Mara imetajwa ni mojawapo ya tatizo linalokwamisha urejeshaji wa uhusiano kati ya uongozi wa mgodi huo na wananchi.

Kaimu Meneja wa mgodi huo, Francis Uhadi alibainisha hayo juzi wakati wa kikao cha baraza la madiwani cha kujadili na kupitisha fedha ya uwajibikaji Sh. bilioni tisa ambazo zimetengwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ili kutekeleza miradi mbalimbali kwa wananchi.

"Sisi kama mgodi tunatamani ukuta uliopo ungeondolewa ili wananchi wanaozunguka mgodi waendelee kufurahia uhusiano mwema ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kufanya biashara. Lakini tunaogopa wavamizi wanaotoka maeneo tofauti ambao hasa sio wazaliwa wa Nyamongo wala Tarime na Mara,"alisema Uhadi.

Hivyo, aliwaomba wananchi hao maarufu kama intruder 'wavamizi' wadhibitiwe kwa kushirikiana na jamii inayozunguka mgodi huo akisema vitendo hivyo vinarudisha nyuma ustawi wa uzalishaji wa shughuli za mgodi huo.

Naye Kaimu Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Tarime Vijijini, Modesta Lema alisema wamepokea mgawanyo wa Sh. biloni tisa ambapo kati ya hizo Sh.milioni 485 zimetengwa kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za miradi ya jamii.

Alisema Sh. bilioni 5.1 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za halmashauri na Sh.bilioni 3.4 ni kwa ajili ya shughuli za vijiji vinavyozunguka mgodi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime, Simioni Kiles alitaka idara hiyo kusimamia ipasavyo matumizi mazuri ya fedha kama ilivyopangwa, ili utekelezaji wa miradi ya wananchi iendelee kwa kasi.

Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, Mwita Waitara aliwaomba watendaji pamoja na madiwani kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha fedha hiyo inatekeleza shughuli za miradi iliyokusudiwa na siyo vinginevyo.

Aidha Waitara alionyesha kukerwa na baadhi ya watu ambao wanapotosha na kukwamisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na kuwataka kuacha tabia hiyo.

## Wasichana wapewa mbinu kukabiliana na ukatili kijinsia

**Na Shaban Njiia,** KAHAMA

WASICHANA zaidi ya 1,000 kutoka mikoa ya Shinyanga na Mara wamepatiwa mafunzo ya afya ya uzazi na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF).

Lengo la mafunzo hayo ni kuwasaidia kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia ukiwemo ukeketaji na mimba za utotoni.

Mratibu wa mradi wa 'chaguo langu haki yangu' unaotekelezwa na shirika hilo kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na Idadi ya Watu (UNFPA), Joyce Kessy alisema licha ya elimu hiyo wanahakikisha pia wanainua uchumi kwa mabinti waliofanyiwa ukatili.

Kessy alisema kuwa tayari mabinti 1,073 wenye umri wa miaka 10 hadi 24 wamefikiwa elimu hiyo ya afya ya uzazi, stadi za maisha na ujuzi mbalimbali kupitia vyuo vya VETA vilivyopo mkoani Shinyanga na Mara, ikiwemo kupatiwa vifaa vya utendaji kazi bure.

"Mradi huu tunafadhiliwa na serikali ya FINLAND na ukomo wake itakuwa mwaka 2025, hivyo kwa mabinti ambao wameshafikiwa na kupelekwa kwenye vyuo vya ufundi wapo 463 kati yao 172 wanatoka Kishapu, 157 Kahama na Mara 134 na tumewapatia vifaa kulingana na kila mmoja alichosoma vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh.milioni 80,"alisema Kessy.

Alisema wazazi wa mabinti hao walioachishwa masomo kwa matatizo mbalimbali wamekuwa na ushiriki mdogo kutokana na kuhitaji mabinti hao waolewe.

Alisema lengo lao ni kujipatia fedha au ng'ombe na wale wenye watoto wenye ulemavu wanawaficha bila kujua ni rahisi kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kulinganisha na wengine.

Kessy alisema licha ya kuwapatia elimu na vifaa vya kazi bure wameingia makubaliano na mabinti, wazazi na maofisa maendeleo ya jamii ngazi ya kata kuhakikisha wanavitumia vifaa hivyo kwenye matumizi yaliyopangwa na siyo kuvikodisha kwa watu wengine na wale watakaobainia hatua za kisheria zitachukuliwa.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Kahama, Swaiba Chemchem alisema mradi huo umetoa mwanga kwa mabinti waliokuwa wamekosa matumaini na kwa sasa wanaweza kutimiza ndoto zao zilikuwa zimefifia.

Makonda anavyogeuka kuwa mtetezi wa watu



Ukurasa 13



Ukurasa 14

# Demokrasia ya makundi CCM iliishia kwa Lowassa

siasa

JUMATANO FEBRUARI 14, 2024

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

## WAKATI MISWADA IKIMSUBIRI RAIS

# Wadau: Marekebisho yamejaa mwingiliano wa katiba, sheria

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 2013 unaandika historia, ndiyo wakati taifa lilianza kuelekea kwenye mchakato wa kuandika katiba mpya.

Katiba ilielekeza nguvu zaidi katika kusikiliza na kukusanya maoni na mapendekezo ya wananchi kupitia Tume ya Jaji Joseph Warioba.

Mambo makubwa yanayopendekezwa na wananchi Bara na Visiwani ni pamoja na kutenganisha mamlaka ya mihimili mitatu ya utawala na pia kupunguzia mamlaka rais.

Muundo wa Muungano, kuwapo tume huru ya uchaguzi na kutoa ruhusa wananchi kupinga matokeo yote ya uchaguzi mahakamani, ni haki wanazozitaka kikatiba.

Katiba mpya ilitaka kuruhusu wagombea huru na uwajibikaji kwenye uteuzi wa watendaji wakuu kwenye taasisi za umma mfano mashirika, mahakama na wakala, ikiwataka waidhinishwe na bunge kwanza.

Aidha, mbali na katiba hiyo kujikita katika kupunguza mamlaka yaliyotwishwa muhimili mmoja au rais, ilipendekeza pia wapigakura (wananchi), kuhoji na kudhibiti wabunge hata kuwawajibisha kama hawatimizi wajibu wao majimboni.

Licha ya kufanyika mkutano wa Bunge Maalum la Katiba, haikupatikana. Hata hivyo, kwa miaka mitatu sasa Watanzania wameamsha tena kilio cha katiba mpya.

Wanataka iwepo tume huru ya kusimamia uchaguzi ili uwe huru na haki, ili mshindi na mshindwa aridhike bila kinyongo.



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana. PICHA: MTANDAO

Wanataka mahakama zisikilize kesi zote za uchaguzi na zitoe haki bila kuendeleza maelekezo ya kisheria kuwa matokeo ya uchaguzi wa rais yakitangazwa hapingwi popote.

Polepole ndiyo mwendo, serikali imefikisha miswada ya sheria zinazohusika na uchaguzi zikiwamo Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sheria ya Tume ya Uchaguzi na ile ya Vyama vya Siasa.

Miswada imejadiliwa bungeni, wadau wametoa maoni na kurudishwa bungeni kupitishwa marekebisho na sasa kinachosubiriwa ni saini ya Rais ili zitungiwe kanuni zianze kutumiwa.

Wadau wanazungumzia mchakato huo, wakisema bado kuna walakini. Kilichofanyika bungeni ni mwingiliano wa sheria na katiba na inavyoelekea sheria zinavunja katiba.

Wakili wa kujitegemea James Marenga, anazungumza na Nipashe kuhusu mkanganyiko, unaotokea akisema kuanzia ibara ya 13 katiba inakataza kuwa sheria yoyote itakayokuwa kinyume na katiba batili.

Akirejea mabadiliko hayo yaliyofanyika hivi karibuni, anasema sheria hizo zinaingilia majukumu ya Rais katika uteuzi mfano katiba inamtaka ateue mwenyekiti wa tume ya uchaguzi, mkurugenzi na makamishna.

"Ni maelekezo ya katiba, sheria ya tume ya uchaguzi inayorekebishwa na bunge, inataja kuundwa tume ya usaili, ambayo kwenye katiba haipo. Huenda Rais atazingatia katiba, kuitetea, kuilinda kwa mujibu wa kiapo chake."

Hata hivyo, anaonyesha wasiwasi kuwa Rais hawezi kukiuka katiba kwa kutekeleza mabadiliko ya sheria yaliyofanywa na bunge, inawezekana mabadiliko yaliyofanyika yasifikie uhalisia.

**KATIBA NI JIBU**

Suzan Lyimo ni mwanasiasa mbobezi na mbunge wa zamani wa CHADEMA, anayesema matarajio ya wadau huenda yasipatikane.

"Mosi ni tume huru ya kusimamia uchaguzi, marekebisho yanaondoa wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi na kumwingiza kwenye watumishi waandamizi..."

Kwa hali hiyo marekebisho hayajaleta tume huru waliyoitaka, bado uchaguzi unaendelea kusimamiwa na watumishi wa umma, anaeleza.

"Ukamweka mtumishi wa umma mwandamizi kitu ni kile kile ni mwajiriwa wa serikali," anafafanua Suzan.

Anakumbusha kuwa tume ya uchaguzi ilishatoa ripoti na kueleza kuwa inahitaji watumishi wake yenyewe, hivyo inashangaza hata takwa la tume halikuzingatiwa.

Anatoa mfano kuwa mwaka 2020 mgombea aliengulliwa akakata rufani akashinda, tume ikamrudisha kwenye uchaguzi, lakini akakataliwa na mkurugenzi (msimamizi) wa uchaguzi.

"Tunataka watumishi wa tume, si wa serikali wawe waandamizi au wakurugenzi wasisimamie uchaguzi ili uwe huru na haki," anasisitiza.

Suzan anasema wanataka upelekwe muswada bungeni utakaoanzisha mchakato wa katiba mpya, badala ya kuleta vipengele vya sheria kama ilivyofanyika.

Mambo mengi ambayo yanahitaji kubadilishwa ili kuwa na uchaguzi yapo kikatiba, mfano ibara ya 74 inasema kutakuwa na Tume ya Uchaguzi, haisemi kutakuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, kama Sheria ya Tume ya Uchaguzi inayosubiri kusainiwa inavyosema. "Haiwezekani kuwa na sheria inayotofautiana na katiba. Tunataka kuwe na mchakato wa katiba mpya. Namshauri Rais asisaini kwanza asikilize maoni ya wananchi. Sheria zirudi tena bungeni zifanyiwe marekebisho. Lakini kikubwa aanzishe mchakato wa katiba mpya."

Anasema hakukuwa na sababu ya kuleta vipande vya sheria na kuongeza 'mkanganyiko' badala ya mabadiliko, akisisitiza ulazima wa kurekebisha katiba.

INAENDELEA UK. 12

# Vita vilivyowageuza wanawake, watoto wakimbizi Gaza

## •Watembea kilometa 20 kwa miguu kusaka hifadhi, magofu sasa makazi

**Na Maulid Mmbaga**

VITA vinavyoendelea baina ya Hamasi na Jeshi la Israel kwenye ukanda wa Gaza mbali na kusababisha vifo, ulemavu na kuharibu miundominu, inatajwa kuwa chanzo wanawake na watoto kuwa wakimbizi wanaotanga tanga kusaka hifadhi.

Wanafananishwa na vifaranga vilivyotelekezwa jangwani wakati wa mvua , matope, vumbi na baridi bila ya kujua pa kukimbilia, kutetea uhai baada ya kushuhudia jamaa zao wakiuawa.

Inaelezwa kuwa baada ya kukwama kwenye jengo kwa zaidi ya wiki moja katika kitongoji cha Gaza City kilichozingirwa na wanajeshi wa Israel, kundi la wanawake na watoto wa Kipalestina walilazimika kukimbilia kusini wakiwaacha wanafamilia wengine nyuma na wengine wakitembea ukanda wa pwani ili kutoroka.

Mmoja wao anasema amemtelekeza jamaa zake ufukweni, akihofia kuwa tangu wakati huo ameshambuliwa na mbwa wanaozurura eneo hilo.

Wengine katika Hospitali ya Martyrs na watoto wao 16, wanasema wamefika katika eneo hilo baada ya kutembea saa nane kwenye mvua na baridi wakitokea Gaza.

Wanadai wanajeshi wa Israel waliwateka nyara waume zao, mwadada mmoja, daktari wa kike na jamaa zao kutoka katika jengo la ghorofa walilokuwa wakijihifadhi, wakishutumu jeshi hilo kwa vitendo hivyo.

Siku chache zilizopita ilionyeshwa video ya jengo kubwa ambalo wanawake wengi wa Kipalestika wanasema kuwa walijifika katika magofu wakihofia usalama wao.

**WAKWAMA MAGOFUNI**

Israa Hassan, mmoja wa wanawake hao anasema kwa wiki nzima kundi hilo lilikuwa limenasa katika ghorofa huko Al-Rimal, akidai jeshi la Israel liliwatisha na kuwatia watoto wao hofu wakiwazingira wiki nzima.

"Hatukuwa na chochote cha kula au kunywa ndani ya nyumba, ni vigumu kupata maji, na ilikuwa maji ya chumvi. Tulikunywa maji chumvi na watoto hatukuweza kupiga kelele kwa hivyo wasingeweza kujua kuwa tulikuwapoe," anasema Israa.

Hoda Harb, mjumbe mwingine wa kundi hilo, anasema askari hao walipofika kwenye jengo walilokuwa wamejificha, walilivamia licha ya kusema kuna watoto ndani. Na kwamba waliwafungulia mlango na kuwataka wasipige risasi huku wakiwaambia kuwa wana watoto, lakini waliendelea kupiga risasi.

Anasema walipoambiwa waondoke, wanajeshi wa Israel walisema jengo hilo litalipuliwa ndani ya dakika 10.

Anaeleza kwamba mwanzoni hawakutaka kuondoka kwenye jengo hilo, lakini jeshi la Israel lilianza mashambulizi makali ya mabomu katika eneo la karibu. Na wakidai kuwa waliharibu lango la jengo na kuingia na kuwachukua wanaume wote na kukusanya watu waliokuwa kwenye ghorofa hiyo kuwapeleka juu.

Anadai kuwa wanajeshi wa Israel waliwapiga na kuwavua nguo wanaume waliokuwa kwenye jengo hilo.

"Walikuwa wakiganda, wamevaa nguo za ndani tu. Baada ya hapo walituomba sisi sote, wanawake wote tushuke ngazi. Wanaume wengi walikuwa wamezuiliwa, Tulisikia vilio vyao kwa sababu walikuwa wakiwapiga," anasema.

Anabainisha kuwa Israel imeweka vilipuzi katika majengo ambayo watu walikuwa wamejihifadhi, akidai kuwa walisikia nyumba zikianguka juu ya vichwa vya watu.

"Walikuwa karibu kutuzika, lakini tuliwasihi watutoe nje. Walitutoa na kuwachukua wanaume kwenye mizinga. Wakatuambia twende baharini hadi Rafah," anasema.

Kwa mujibu wa wanawake hao, safari ya miguu waliyotembea ilikuwa ni zaidi ya kilomita 20 maili 12, na kwamba matembezi mengi yalikuwa kwenye mchanga chini ya pwani.

**KAULI YA UN**

Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kibinadamu Volker Türk, anasema majeshi ya Israel yanabomoa makazi na majengo mengine ya kiraia vitongojini mjini Gaza.

Inaelezwa kuwa kitongoji cha Al-Rimal mjini Gaza kimeharibiwa na kampeni kali ya Israel ya kulipua mabomu, iliyozinduliwa kujibu mashambulizi mabaya ya Hamas dhidi ya Israel Oktoba mwaka jana.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya inayoongozwa na Hamas huko Gaza hadi sasa zaidi ya Wapalestina 28,000 wameuawa na 66,000 tangu vita ilipoanza.

**UTETEZI WA ISRAEL**

Jeshi la Israel (IDF) linapoulizwa kuhusu tuhuma hizo linajibu kuwa vikosi vya taifa hilo vilikuwa vikifanya kazi katika ngome za Hamas kama sehemu ya juhudi za kusambaratisha uwezo wa kijeshi wa kundi hilo na kuwaokoa mateka wa Israel waliowateka.

Pia linasema wanawahamisha wananchi kutoka maeneo ya mapigano na kuwapeleka sehemu salama, na kwamba mashambulizi yao yanatekelezwa kwa kuzingatia taarifa za kijasusi kuhusu miundombinu ya kigaidi.

"Watu wanaoshukiwa kuhusika na ugaidi wanazuiliwa na kuhojiwa. Watakaobainika kutoshiriki katika shughuli za kigaidi wanaachiliwa huru, wale waliowekwa kizuizini walitendewa kwa mujibu wa sheria za kimataifa, na upekuzi ulikuwa ni muhumu kufanyika mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa hawakuficha vilipuzi au silaha nyingine.

# Wadau: Marekebisho yamejaa mwingiliano wa katiba, sheria

INATOKA UK. 11

"Mathalani, sheria inayosubiri kusainiwa ina kamati ya usajili yenye wajumbe, majaji wakuu wa Zanzibar na Bara na ambao ni wateule wa Rais. Tunataka iwe na wajumbe huru mfano viongozi wa dini, vyama vya siasa, AZAKI.

"Kamati hii ndiyo msingi wa kuteua wajumbe wa tume huru ya kusimamia uchaguzi. Lakini marekebisho bado inaweka wateule wa Rais, tume hiyo inawezaje kuwa huru isimamie uchaguzi kwa haki?" Anahoji Suzan.

Dokta Peter Kafumu, mbunge wa zamani wa Igunga CCM, anapozungumzia kufikiwa marekebisho hayo na sasa kuelekea kuwa sheria, anasema mengi yanayojadiliwa na kuhitaji kubadilishwa yapo kikatiba zaidi.

Anakumbusha kuwa msingi wa sheria hizo upo kikatiba na kwamba mabadiliko yamefanyika lakini, kuna hitaji la kuiangalia tena katiba.

**CCM IKAE PEMBENI**

Askofu Profesa Victor Chisanga, pamoja na kuhubiri habari njema, ni mchambuzi wa siasa za ndani na kimataifa, anayesema marekebisho ya sheria hizo, hayaleti uwezekano wa kuwa na uchaguzi uhuru, wa haki na unaokubalika.

Profesa Chisanga, Askofu wa Kanisa la the World United Alliance Church in Tanzania (WUACTz), anakumbusha kuwa miswada hiyo imejadiliwa na kupitishwa na wabunge wa chama kimoja, ambao hawakubali kuwa na tume huru ya uchaguzi au sheria za uchaguzi ambazo zinaweza kuleta ugumu kwa upande wao.

Profesa Chisanga mhadhiri mstaafu wa Chuo Kikuu cha Ardhi, anaona kuwa wabunge wa chama kimoja hawawezi kubadilisha sheria hata katiba kwa vile wanataka ziwalinde.

"Marekebisho yote yanayofanywa na bunge kwa wakati huu wakiwa wote ni chama kimoja yanaacha maswali. Ni kama hawako tarayi kunyoosha mambo, wakihisi yatawaweka pembeni," anasema Profesa Chisanga.

Anazungumzia ibara ya 74 ya katiba inayoweka muundo, uteuzi na uendeshaji wa uchaguzi.

Aidha, anasema marekebisho hajahusisha wagombea binafsi kama ibara za 39(2) na 67(1) za katiba zinavyowazuia.

Askofu Profesa Chisanga anasema kwanza ni katiba, lakini haijabadilishwa kwa sababu ina maslahi ya kutetea chama kiendelee kuwa madarakani.

"Kuendelea kujitetea huko hakuna faida kwa taifa linalotaka katiba ili kuwe na haki, maridhiano na ukweli nyakati zote zikiwamo za uchaguzi."

"Naona marekebisho ya sheria ya NEC, vyama vya siasa na hata katiba bado, vyema yafanywe na wadau wengine na vyama vya upinzani. CCM ikae pembeni. Nasema haya kwa sababu wanaonekana kuwa na hofu na hatima yao."

Anakumbusha kuwa tume huru ya uchaguzi na sheria zisizolalamikiwa zitasisimama kwa ajili ya vyama vyote na nyakati zote za uchaguzi kwa maslahi ya taifa, hivyo hakuna haja ya kuiogopa.

Anakumbusha kuwa licha ya kufanyika marekebisho hayo NEC bado inaonekana kuwa na mkono wa CCM kwenye uteuzi wa viongozi akisema ni kama bado hakuna mabadiliko.

Akizungumzia sheria za uchaguzi na hata za tume ya uchaguzi, anasema bado hakujawa na utayari wa kuiacha iwe huru ifanye kazi kwa misingi ya uwazi, akisema bunge hajalileta mabadiliko na huenda haliko tayari kubadilika.

Anaitaka serikali kujitafakari, akiielekeza kuutazama umati unaomiminika kwenye mikutano ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, kueleza kero.

"Hiyo ndiyo hali ya Watanzania kila mtu ana kilio, viongozi wanafanya nini kila mahali ni kero, malalamiko na kero? Tuiache CCM iwe kama ilivyo," anaongeza.

Anavizungumzia vyombo vya dola hasa polisi, mahakama na usalama wa taifa viwe na hekima vitumike kufanya mambo yanayolinda haki, mfano visimamie amani na usalama na kura za wananchi zilizochagua viongozi wao kwa haki.

"Vyombo vya dola visiwe sehemu ya kusababisha wananchi kuendelea kulalamikia matokeo. Mahakama ni chombo cha dola cha kusimamia haki, kinakubali na kusimama kuwa matokeo yakitoka na kutangazwa hakuna kuyabatilisha yanatangazwa kama yalivyo kwanini?" anaongeza na kuhoji Askofu Chisanga.

"Hivi katiba ikisema hakuna kufikishwa popote matokeo hayo mbona hakuna haki hata kwenye kura walizopiga wananchi kumchagua kiongozi wao. Ni vigumu kuwa na uchaguzi huru, haki na unaokubalika katika mazingira haya japo bunge limefanya na kupitisha marekebisho."

Anasema kwa miswada hiyo inayosubiri kusainiwa kuwa sheria bado mchakato wa uchaguzi wa urais hautaweza kuhojiwa mahakamani, kama ambavyo ibara ya 41 (7) ya katiba inavyoelekeza, akihoji "kimefanyika nini sasa?"

Mkurugenzi mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anazungumzia marekebisho yaliyopitishwa, akisema yanaakisi kuwa si kura pekee zinazompa mgombea ushindi.

"Walioyapitisha wana uhakika kura siyo kauli ya mwisho ya kuamua nani ashinde uchaguzi. Mchakato uliofanyika bungeni kwenye sheria hizo haujaweka mazingira ya kuwa na uchaguzi huru na haki kwa sababu sheria hazijaweka mazingira hayo."

Mwanasheria, wakili na mtetezi wa haki za binadamu Hellen anaona bado sheria hazijatengeneza mfumo wa kuufanya uchaguzi uwe huru, haki na unaokubalika.



Ndivyo wananchi walivyokusanyika kwenye mikutano ya hadhara kwa maandamano kumsikiliza Paul Makonda. PICHA: BEATRICE SHAYO

# Makonda anavyogeuka kuwa mtetezi wa watu

**Na Beatrice Shayo,** aliyekuwa RUVUMA

ZIARA ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, inafungua ukurasa mpya wa uwajibikaji na kukosolewa.

Ni kwa vipi? Ziara hiyo inayoanza Januari 19 mwaka huu kutembelea mikoa 20, kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi na kutatua kero za wananchi, imewapa wananchi ari na ujasiri wa kuwataja na kuwahoji watendaji serikalini wanaoshindwa kutatua kero zinazowatesa wapigakura.

Makonda, anaitaja safari hiyo kuwa ina 'staili' ya kipekee ambayo mwananchi anapewa kipaza sauti kumhoji aliyemcheleweshea majibu na utatuzi wa kero yake.

Anawakutanisha ana kwa ana viongozi na wananchi, wanaolalamika, akiwaita mbele ya umma, wanaolalamikiwa kutoa majibu kueleza inakuwaje shida za wananchi hajashughulikiwa.

Hatua hiyo inawafurahisha watu wanaoshangilia huku Makonda akiwaahidi kuwa upande wao na endapo wakiwahoji maswali machache atawaongezea mengine hata kama ni mkurugenzi atawapa maswali na namna ya kumhoji ili wapate majibu ya changamoto zinazowakabili.

Makonda anasema anachokitaka ni haki kutamalaki ndiyo maana hawahutubii wananchi, bali kuwapa nafasi kueleza wapi hawatendewi sawa ili chama kiingilie.

"Chama kimekuja na staili mpya unamhoji unayemtaka utazungumza naye katika huu mkutano na kumuuliza mubashara kero yako na pia nitakusaidia kuhoji maswali kama unazungushwa na utapata majibu yako hapa," anasema Makonda.

Katika ziara hiyo anawasaidia baadhi ya wananchi kuwahoji watendaji huku akiwataka kuwapa ufumbuzi wa kero zao wala si majibu yenye matumaini.

Anawabana kwa maswali watendaji wa serikali na kuwataka kutatua shida za wananchi kwa wakati badala ya kuwapiga danadana na kuwafanya waishi kwa majonzi.

"Wapo viongozi mnawakimbia wananchi wanapowafuata katika ofisini zenu kwa vile mnawaona ni wanyonge, hawana ndugu serikalini au kwa vile ni maskini, leo mtawapa majibu kama Mkuu wa Wilaya ulikuwa unamkimbia mwananchi jiandae," anasema Makonda.

Wananchi hao baada ya kuwasilisha kero zao, Makonda anabaini watendaji ni kikwazo akatoa kipaumbele kwa mwananchi kwenda kupanda gari la mkurugenzi na kukaa kiti mbele kwa ajili ya kupelekwa ofisini kwake ili kutatua changamoto yake.

Kitendo cha kusikiliza wananchi na kuelekezwa kupanda magari ya viongozi hao kiliwaheshimisha na kujiona ni miongoni mwa wenye thamani kwenye jamii.

Makonda anawajulisha watendaji kuwa wapo kuwahudumia Watanzania na haiwezekani wafanye kazi kwa mazoea kwa kuwa ofisi zimewekwa kwa ajili ya wananchi na kuwaonya wasiwakimbie.

Anasema wapo baadhi ya watendaji ni wabovu na kujiona ni miungu watu, atawasilisha ripoti kwa mamlaka za uteuzi ili kutathmini utendaji wao wa kazi iwapo wapo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi au kuangalia maslahi binafsi.

Makonda akisikiliza kero hadi saa 1:30 usiku huku wananchi wakitaka asiondoke na wakinyoosha mikono kupewa kipaza sauti wakiamini ndiye msaada wao, amekutana na migogoro ya ardhi na kunyimwa haki.

Anawataka viongozi wajitathmini kupitia kero hizo namna ambayo wananchi wanafurika kutaka kupatiwa majibu ikionyesha ni namna gani hawawajibiki.

Makonda anawaagiza watendaji wa serikali katika mikoa kufungua kliniki na kuweka watendaji wa kila idara ili kuwasikiliza wananchi ambao walikosa nafasi ya kupata kipaza sauti kuzungumza.

**AREJESHEWA MALI**

Mkazi wa Mpanda mkoani Katavi, Oscar Selemani, anaandika historia kwenye ziara hiyo.

Anasema alikuwa na shamba lenye madini aliyoyagundua tangu 1992, akapewe leseni lakini wakajitokeza watu wenye tamaa ya utajiri wa haraka haraka wakapewa leseni za magendo wakavamia shambani licha ya kwamba hawatambuliwi na serikali ya kijiji.

"Hii kliniki ya Makonda imebaini leseni hizo ni feki wameniambia wenyewe tembea kifua mbele nikaendelee na shamba langu hapa naenda kupiga kazi. Nimefurahi maana nilikuwa ninateseka, leo haki yangu imerejeshwa."

Anasifu anachokifanya Makonda, kuwasaidia wanyonge kitawaamsha watendaji wa serikali kuwajibika na kuthaminiwa na wananchi.

"Unakwenda kwenye ofisi hizo kila mara unapigwa Kiswahili hata wakiwapo unaambiwa hayupo wenye nguvu ndiyo wanahudumiwa sisi wanyonge tunateseka katika hizi halmashauri haki yako kuipata imekuwa ni changamoto kwa hiki anachokifanya Makonda kitaongeza uwajibikaji."

Anasema mfano ni kama hivyo alivyopewa haki yake kwa muda mfupi bila Makonda shamba lake lingechukuliwa na hao wenye fedha, anasema Seleman.

**KUKATA RUFANI**

Makonda anasema chama kimetoa nafasi kwa wananchi kukata rufani pale wanapoona kero zao hazitatuliwi na watendaji wa serikali na kwenda Ofisi za CCM kuwajulisha ili zifanyiwe kazi.

Anasema chama kipo kwa ajili yao, hivyo wanavyofanyiwa figisu katika kudai haki zao wafike katika ofisi za CCM watasaidiwa bila kusumbuliwa.

"Viongozi wetu wa chama watapokea kero yako na kuifuatilia na kama kuna mtendaji amekufanyia ubadhirifu tutapatiwa taarifa na haki yako utaipata ndio maana tumewaomba wananchi wetu kukata rufani katika chama chetu tumejipanga kwa ajili yao," anasema Makonda.

Juma Mapunda anayeishi Songea mkoani Ruvuma anasema watendaji wamekuwa wakiwaita na kuwataka wasipeleke kero zao katika mkutano wa Makonda badala yake watazitatua baada ya kuzipitia.

"Wametuita sisi ambao tuna kero na kutuomba tusiseme matatizo yetu katika mkutano wa Makonda na kutuahidi watazitatu baada ya ziara kuisha sasa hatujui ni kweli watatusaidia au wametudanganya," anasema Mapunda.

Anasema changamoto yake ipo kwenye ofisi za ardhi hazisikilizi wananchi na waliposikia Makonda anakuja wakaitwa mapema na kuahidiwa kuwa zitatuliwa, hivyo wasichukue kipaza sauti kuuliza maswali.

Mkazi wa Mtwango mkoani Njombe, Zulu Nyingo, anasema walikuwa na migogoro wa ardhi ambayo watendaji wanaujua ni wa muda mrefu ambao ni shule ya wazazi ya sekondari Mtwango ambayo imerudishwa mikono mwa serikali.

Anasema awali ilichukuliwa ardhi ya kijiji kwa sababu ya kitega uchumi cha shule kwa sasa imerudishwa mikono mwa serikali, hivyo wanataka maeneo waliyoyatoa yarudi mikono mwa wana kijiji.

Nyingo anasema kinachowauma yupo kigogo katika halmashauri yao anayakodisha maeneo hayo na kujipatia fedha wameitwa na kunyamazishwa wasiongelee hilo tatizo katika mkutano wa Makonda na kuambiwa suala hiyo watalimaliza.

**HADI KWA RAIS**


Makonda anaahidi kuwasilisha ripoti kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa fulani hafai kwa kuwa wamewakuta wananchi wanateseka kupata haki zao.

Anasema zipo changamoto ambazo hazihitaji kusubiri viongozi wa kitaifa kuja kuzitatu na badala yake watendaji wamekuwa kikwazo kwa wananchi na kuwachelewesha kupata haki yao.

## JUKWAA LA UONGOZI

# Demokrasia ya makundi CCM iliishia kwa Lowassa

**Na Ani Jozeni**



EDWARD Lowassa ametutoka, akikaribia umri wa miaka 71 kama angemaliza wiki moja ya mwezi Mei. Kama walivyo watu wengine waliofikia kiwango kikubwa cha umashuhuri unaoweza kusema alifanya kazi kubwa zaidi ya kufikia ndoto zake kuliko idadi kubwa au watu, hata walio mashuhuri.

Kuna eneo moja ambalo amefikia ngazi ya viongozi wachache wa kisiasa hapa nchini, ambao licha ya kukulia katika mfumo na kufaulu wakiwa ndani yake, walitumia ushawishi wao binafsi na kwa hayati Lowassa ukaongezeka uwezo wa kujitegemea kifedha na kuweza kuutingisha mfumo.

Katika vipengele kadhaa kuhusu maisha yake ya kisiasa, Lowassa alifikia kilele cha uwezekano wa ubunifu na mbinu binafsi kama njia ya kuinuka na kujizatiti kisiasa, njia ambayo ilishaonekana kwa mfumo mzima na ikaanza kuleta wasiwasi.

Ilikuwa na pande mbili, mmoja ukiwa ni uhuru wa kuunda makundi ndani ya chama tawala kwa kujiandaa kupata mgombea pale awamu ya mihula miwili inapomalizika.

Eneo jingine ni mabadiliko ndani ya CCM mwanzoni mwa miaka ya 1990 ya kuondoa 'miiko ya uongozi' iliyowekwa mwaka 1967 katika Azimio la Arusha, kuhusu utajiri.

Maisha ya kisiasa ya Lowassa ni kielelezo cha mvutano kati ya kulelewa na chama na kukitegemea kwa msingi wa hofu kwa kiongozi au serikali iliyoko madarakani, halafu hulka ya kujitegemea mwenyewe, kuunda chama ndani ya chama.

Ukweli ni kuwa demokrasia ya vyama vingi haifanyi kazi kwa kila mtu kukitegemea chama, ila kutumia nyenzo zake mwenyewe kufanikisha malengo yake ya kisiasa.

Vyama siyo familia ambako kuna utii ila masoko au magulio ya kisiasa ambako mtu anapeleka utashi wake kisiasa na nyenzo alizo nazo, kujaribisha ndoto zake.

Kabla ya kuendeelea, nikumbushie ngazi kadhaa katika historia ya siasa hapa nchini, kwa waliolelewa, kukulia katika mfumo wakautingisha na kupata matokeo kadhaa, mara nyingine ambayo si mema na kwingineko kuonekana kufaulu.

Mara tu baada ya uhuru mwaka 1962, ilipopitishwa sheria ya kuweka watu kizuizini endapo wanahatarisha usalama wa taifa, Balozi Christopher Kasanga Tumbo aliyekuwa balozi Uingereza, alijiuzulu kurudi kupingana na sheria hiyo. Hata hivyo, alizuiliwa, hadi mfumo wa vyama vingi ulipokubaliwa miaka 30 baadaye.

> Kura za mgombea huyo mara zinapanda na kushuka hasa kwa kuwa amevunwa kutoka CCM; utashi wake kitaifa unatumiwa kuujenga upinzani, na siyo kuiondoa CCM madarakani.

Kiongozi mwingine aliyefikia ngazi ya juu ya kutingisha mfumo alikuwa Oscar Kambona, akiwa Waziri wa Mambo ya Nje mwanzoni mwa 1967, akatofautiana na Azimio la Arusha akahamishiwa Tawala za Mikoa ila nako akakwama kuisemea serikali kikamilifu, akaondoka nchini.

Jitihada zake dhidi ya mfumo ingebidi zitokee kwingine kwani hakuwa na pa 'kukanyaga' ili apambane na mfumo kutoka ndani, alikwama hadi aliporudi 1992.

Wako wengine takriban wawili waliomtangulia Lowassa katika jitihada yao kutikisa mfumo kwa ushawishi binafsi, yupo Edward Sokoine, Waziri Mkuu, Januari 1983.

Akatangaza mpango wa kupambama na wahujumu uchumi ukaanza kuleta simanzi katika sekta ya biashara kwa jumla. Mwalimu Julius Nyerere, wakati huo Rais, akauzuia, halafu mageuzi ya uchumi yakaanza taratibu kwa kuingizwa daladala na baadaye ikaja mitumba na maisha yakaendelea.

Aliogopewa asije kumrithi Nyerere, akapata ajali barabarani Dakawa mkoani Morogoro na kufariki dunia.

Aliyefuata miaka takribani 12 baadaye alikuwa Augustine Mrema (sasa marehemu), ambaye alitumia nafasi ya uwaziri wa Mambo ya Ndani kuibua kashfa ya ukopeshaji fedha na kutaja watuhumiwa dawa za kulevya, akaondolewa cheo cha Naibu Waziri Mkuu na kuhamishiwa Wizara ya Kazi, akahamia upinzani NCCR-Mageuzi kabla ya upinzani wa 1995.

Alipata wabunge takribani 16 akiwa upinzani, walipokosana naye uchaguzi wa 2000 akagombea kupitia TLP, chama hicho kikadidimia, hadi leo.

Ni kanuni kuwa kuhamia upinzani kwa kiongozi mwenye ushawishi chama tawala, halafu umma upate picha kuwa ameonewa, anakuwa ngome mahiri ya upinzani na kuwa kimbilio.

Ndiyo hapo kuhamia CHADEMA kwa Lowassa mwaka 2015, alifanikiwa kukipatia chama hicho wabunge zaidi ya 70, wakati mhamiaji mwingine kutoka CCM (ambako hakuwa na mizizi halisi) Dk. Wilibrod Slaa, ambaye hata hivyo alishakuwa mwenyeji upinzani, alipata viti 26 mwaka 2010.

Kuna tofauti za kimfumo zinazoamua hatima ya mwanasiasa na athari kwa mfumo wenyewe pale anapokuwa na utashi (charisma) inayozidi nafasi aliyopewa na chama (hapa ikiwa ni pamoja na nafasi au dhamana serikalini). Tofauti hizo ziko bayana katika kuondolewa CCM na kujiunga na upinzani kwa Seif Sharif Hamad kuanzia miaka ya 1980 hadi mwanzo wa miaka ya 1990.

Hamad alijiunga na CUF kama Katibu Mkuu, na kiongozi muhimu wa chama hicho hasa kwa upande wa Zanzibar ambako alikuwa ndiye mwenyekiti.

Kulikuwa na mazingira ya upinzani wa kina yaliyomwezesha Maalim Seif kuwa kiongozi wa kulingana na utawala uliopo, tofauti na Mrema au Lowassa Bara kulikokuwa na upinzani wa kudakiza na chaguzi za chama kimoja.

Kura za mgombea huyo mara zinapanda na kushuka hasa kwa kuwa amevunwa kutoka CCM; utashi wake kitaifa unatumiwa kuujenga upinzani, na siyo kuiondoa CCM madarakani.

Kwa maana hiyo Lowassa alikuwa kielelezo bora cha kutumia fursa ndani ya chama kutokana na uhuru mpana uliokuwapo na halafu chama kikashindwa kubeba athari za utashi huo.

Mgombea aliyetokana na mitafaruku ndani ya chama alipopata madaraka alijitwika kazi maalum ya kuvunja ngome za utashi binafsi kupangua maeneo ya kiutendaji na hata kibiashara ambayo yaliwezesha watu kama Lowassa kufikia ngazi ya juu ya ushawishi na kuendelea na jitihada zao, bila kukitegemea chama.

Baada ya uchaguzi mkuu 2015 kupita ambako CCM ina mgombea tayari, ni kizazi cha wagombea wa 2030 kitakachothibitisha kama kuna uhuru mpana ambao kwa jumla umeanza kurudi katika kipindi cha 'maridhiano'.

Hata hivyo, haifahamiki utafikisha chama tawala katika hali gani, ila CCM haitakuwa rahisi kuvutwa kwa kumfuata mtu mmoja kwani nguvu ya taasisi na taratibu rasmi inaongezeka sasa.



# 95% ya wanawake w'biashara Dar waombwa rushwa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa shirika la Women and Social Protection (WSP), Dk. Flora Myamba, amesema asilimia 95 ya wanawake 3,884 wanaomiliki biashara na kampuni jijini Dar es Salaam wamekiri kuombwa rushwa.

Amesema wanawake hao wamekiri kuombwa rushwa wakati wa kufuatilia zabuni kwenye sekta ya manunuzi ya serikali, ikiwemo rushwa ya ngono.

Dk. Myamba aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza kwenye warsha ya watumishi wa umma kuhusu matatizo ya wanawake kushiriki kwenye zabuni za ununuzi serikalini iliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema kuwa wanawake zaidi ya 3,884 wanaomiliki biashara na kampuni jijini Dar es Salaam wamekiri kuombwa rushwa wakati wa kufuatilia tenda kwenye sekta ya manunuzi ya serikali ikiwemo rushwa ya ngono.

Alisema wanawake wanaomiliki biashara na kampuni nchini wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kwenye kuomba zabuni za ununuzi serikalini ikiwemo kuombwa rushwa ya ngono.

Dk. Myamba alisema kuwa pamoja na asilimia 70 ya bajeti ya serikali inakwenda kwenye manunuzi ya umma, lakini kundi kubwa la wanawake wajasiriamali limeachwa nyuma kwenye kuomba tenda hizo.

Alisema wanawake wengi hawajapata fursa ya kushiriki kwenye manunuzi ya umma na hivyo wameshindwa kujiongezea kipato kwenye biashara zao kutokana na kutokuwa na uelewa pamoja na mitaji midogo.

Dk. Myamba alisema kutokana na changamoto hiyo shirika la WSP liliamua kufanya utafiti wa kujua ni namna gani kundi la wanawake wafanyabiashara na wenye kampuni wananufaika na zabuni zinazotangazwa kwenye manunuzi ya serikali ambapo waligundua kuna ushiriki mdogo wa wanawake hao.

Alisema utafiti walioufanya kwenye wilaya zote tano za mkoa wa Dar es Salaam ambapo jumla ya wanawake wafanyabiashara na wenye kampuni ni zaidi ya 3,884 na walihojiwa na wengi wao hawakuwa na uelewa kuhusiana na zabuni za manunuzi ya serikali.

"Kutokana na utafiti huo tumebaini kuwa vitendo vya rushwa vimeshamiri kwenye sekta hiyo kwa sababu asilimia 95 ya wanawake waliohojiwa walikiri wengi wao kuombwa rushwa wakati wanafuatilia hizo tenda za manunuzi serikalini," alisema.

Alisema warsha hiyo imewakutanisha watumishi wa umma kutoka wizara zote nchini ambao wanajishughulisha na masuala ya kijinsia pamoja na ugavi ili kuzungumza nao na kupata majibu ya namna bora ya wanawake kushiriki fursa ya manunuzi serikalini.

Naye, Mkurugenzi wa uzuiaji rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Sabina Seja alikiri taasisi hiyo kutofanya utafiti kwenye sekta ya manunuzi yanayohusu ushiriki wa wanawake.

Alisema kuwa utafiti unaofanyika zilihusu masuala mengine ambayo hajajikita kwenye ushiriki wa wanawake kwenye manunuzi ya umma na kusema kuwa hiyo ni changamoto kwao kwani wamepata hatua ya kuanzia.

Akizungumzia kuhusu rushwa ya ngono alisema kuwa ni mchakato wa muda mrefu na wa siri baina ya mwombaji na mtoa rushwa, hivyo siyo rahisi kuigundua kama wanaohusika hawatatoa taarifa.

Alisema kwa upande wa rushwa ya ngono inafanyika kwa siri na ni wachache sana ambao huwa wanatoa taarifa kwenye taasisi yao.

Mkurugenzi wa kampuni ya usafi na uondoshaji wa taka ngumu ya Saki iliyopo Jijini Dar es salaam, Sophia Nyang'oro alisema kuwa chanzo cha rushwa ya ngono kwa wanawake ni kutokuwa na uelewa kuhusiana na tenda zinazotangazwa na serikali.

Alitaja sababu nyingine kuwa ni kutokuwa na mitaji pamoja na uwezo wa kuendesha tenda hizo, hivyo wanajikuta wakitoa rushwa ya fedha au ya ngono ili waweze kupata huku wakijijua kuwa hawana uwezo na kuendesha tenda hizo.

## Watoto yatima nyumba ya matumaini waomba bima ya afya

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATOTO yatima wa Kituo cha Nyumba ya Matumaini Miyuji jijini Dodoma, wameiomba serikali, taasisi za kidini, mashirika, watu binafsi na makundi mbalimbali kuwasaidia bima ya afya, ili waweze kupata huduma katika hospitali mbalimbali nchini.

Ombi hilo lilitolewa juzi na mlezi wa kituo hicho, Sister Inviolata Francis alipokuwa akizungumza kwa niaba ya watoto wa kituo hicho, baada ya kupokea misaada iliyotolewa na wanafunzi wa chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kwa kushirikiana na waumini kutoka The Church of The Lord Jesus for All Nationas Tanzania.

Sister Inviolata alisema kuwa watoto wa kituo hicho pamoja na changamoto wanazokabiliana afya imechukuwa nafasi ya kwanza kutokana na kukosekana kwa matibabu yaliyo sahihi ya huduma ya kiafya.

Alisema kuwa kituo kina watoto 71 ambao wanaishi kwa kutegemea misaada, wapo wanaosoma shule ya awali, msingi na sekondari kwa msaada wa wahisani.

Naye mratibu wa kikundi hicho cha wanafunzi wa chuo pamoja na kanisa, Nancy Kazimoto, alisema kuwa misaada iliyotolewa lengo ni iweze kuwasaidia kupunguza changamoto wanazo kabilianazo kwenye maisha yao.

Kazimoto alisema kuwa wanafunzi hao wamekuwa wakijitoa kutoka kwenye mapato yao kwa ajili ya watoto yatima wanaolelewa kwenye vituo, ili waweze kujimudu hivyo wamewaomba wahisani wengine kujitokeza katika kusaidia.

Alitaja misaada iliyotolewa kwenye kituo hicho ni pamoja na sukari, sabuni, mafuta ya kupakaa na ya kula, dawa za miswaki, madaftari, peni na penseli, mchele, pipi na biskuti.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akitia saini kitabu cha maombolezo ya kifo cha Waziri Mkuu mstaafu, Edward Ngoyai Lowasa, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## DC: TEHAMA itumike katika masomo yenye uhaba walimu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Paskasi Muragili amezitaka shule za msingi na sekondari kuchukua hatua katika ufundishaji kwa njia ya TEHAMA kwa masomo yenye upungufu wa walimu, ili kuinua kiwango cha elimu wilayani hapa.

Alitoa agizo hilo jana katika kikao kazi cha kupokea taarifa ya hali ya ufundishaji kwa njia ya TEHAMA katika Halmashauri ya Wilaya Singida na Manispaa ya Singida.

Alisema idadi ya shule ambazo zimeanza utekelezaji tangu kutolewa kwa maelekezo ya kufundisha kwa njia ya TEHAMA Oktoba 4, 2023 hairidhishi, hivyo kutoa agizo kwa wakurugenzi kuhakikisha kila halmashauri inanunua vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kufundishia wakati kila shule ikijipanga kununua vifaa vyake.

"Wakurugenzi nunueni vifaa hivyo ambavyo kwa sasa vitakuwa vikizunguka kwa kila shule wakati shule zikijipanga kupata vifaa vyao, shirikisheni wazazi kupitia vikao na mikutano na wafadhili ili kufanikisha upatikanaji wa vifaa," alisisitiza.

Jumla ya shule za sekondari nane na za msingi 13 zimeanza kutekeleza ufundishaji kwa njia ya TEHAMA katika halmashauri hizo.

Wakiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa agizo hilo, maofisa elimu wa divisheni za elimu sekondari na msingi wameeleza changamoto kubwa iliyowakwamisha na kusababisha kusuasua kwa utekelezaji wa agizo hilo ni ukosefu wa vifaa vya TEHAMA

Naibu Meya wa Manispaa ya Singida, Geophrey Mdama aliunga mkono agizo hilo na kusema ni wakati sasa wa kuamka na kutekeleza kwa vitendo kwani inawezekana kupitia njia shirikishi jamii.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Elia Diga alisema agizo hilo wamelipokea na linakwenda kutekelezwa kwa ushirikiano baina ya wataalam, wazazi na wanasiasa kwa maana ya madiwani.





# Watoto 94,343 kupatiwa chanjo ya surua, rubella

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATOTO 94,343 wenye umri wa kuanzia miezi tisa hadi miaka mitano mkoani Njombe wanatarajiwa kupata chanjo kwa ajili ya kuwakinga na magonjwa ya surua na rubella.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari, aliyasema hayo wakati wa kikao cha kamati ya afya ya msingi ya dharura kwa ajili ya kujadili magonjwa ya mlipuko yanayoendelea kutokea nchini na hamasa juu ya kampeni ya surua na rubella itakayofanyika Febuari 15 hadi 18 mwaka huu.

Omari alisema wataalamu wanapaswa kuimarisha usimamizi wa utoaji huduma za chanjo katika kipindi cha kampeni na kutoa majibu ya kitaalamu pindi inapotokea upotoshaji ili kuepuka tamalaki.

Aidha, aliwataka wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri mkoani humo kusimamia utoaji wa chanjo katika maeneo yao ili kuweza kuleta tija.

"Mtoto asiyepata chanjo ni hatari kwa maisha yake na kwa jamii inayomzunguka kwani anaweza kuambukizwa au kuwaambukiza wengine ugonjwa kutokana na kutokuwa na kinga," alisema Omari.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Dk. Juma Mfanga, alisema chanjo hiyo inatolewa kwa watoto wenye umri wa miezi tisa hadi 18 ili kupata kinga kamili.

"Kila mtoto anatakiwa kupata dozi mbili, dozi ya kwanza ya chanjo ya surua na rubella hutolewa akiwa na miezi tisa baada ya kuzaliwa na dozi ya pili atapata baada ya kutimiza miezi 18 tangu kuzaliwa kwa utaratibu wa kawaida," alisema Mfanga.

Alisema kisayansi kinga dhidi ya chanjo hupungua baada ya miaka mitatu na hivyo utaratibu wa kufanya kampeni unalenga kuongeza kinga ya mwili kwa watoto waliokamilisha ratiba za chanjo.

Alifafanua kwamba mwaka 2023 Mkoa wa Njombe ulikuwa na wahisiwa wa ugonjwa wa surua wapatao 63 kati yao wagonjwa 27 sawa na asilimia 47 waligundulika kwa vipimo vya maabala kuwa wanaugonjwa huo.

"Halmashauri tano za Mkoa wa Njombe zilipata mlipuko wa surua na rubella isipokuwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa pekee," alisema Mfanga.

Naye mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI, Jeremia Mwandaje, alisema lengo la kampeni hiyo ni kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa surua.

"Tunatoa chanjo katika hali ya kawaida kwenye vituo vyote vya afya lakini tunatoa chanjo kwa njia ya kampeni, katika kutoa chanjo kwa njia hizo zote kuna watoto ambao hatuwafikii na kuna sababu mbalimbali za kutowafikia hawa watoto," alisema Mwandaje.

Mwandaje alisema kuwa kutokana na ugonjwa huo kuna baadhi ya wazazi wanakuwa wanawapaka matope au majivu kwenye miili yao wanapoona dalili za vipele hali inayosababishwa na kukosa elimu sahihi ya kutibu na kushughulikia tatizo hilo.



Meya wa Jiji la Mbeya, Sheikh Dor-Mohamed Issa, akizungumza wakati akifungua Kikao cha Bajeti cha Baraza la Madiwani wa jiji hilo, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Malalamiko 34 yawasilishwa TAKUKURU miezi miwili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RUSHWA imetajwa kuwa bado ni kikwazo kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali mkoani hapa, kwamba katika kipindi cha Oktoba mpaka Desemba mwaka jana, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilipokea malalamiko 34 yanayohusu vitendo hivyo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Maghela Ndimbo, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya taasisi hiyo katika kipindi cha miezi mitatu.

Alisema katika kipindi hicho walipokea malalamiko 94 ambayo yalikuwa yanahusu masuala mbalimbali na kwamba kati yake 34 ndiyo yalikuwa yanahusu vitendo vya rushwa.

Alisema katika kipindi hicho taasisi zilizoongoza kwa kulalamikiwa na wananchi ni idara ya ardhi, utawala, fedha na afya na kwamba malalamiko hayo yanaendelea kuchunguzwa na yapo katika hatua mbalimbali.

"Katika kipindi hicho Jamhuri ilishinda mashauri yote matatu ambayo yalikuwa yanaendelea kwenye mahakama mbalimbali za mkoa wetu na kufikia mwishoni mwa Desemba mashauri 23 yalikuwa yanaendelea mahakamani," alisema Ndimbo.

Alisema wanaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo utoaji wa elimu ya rushwa kwa wananchi ikiwamo programu ya 'TAKUKURU RAFIKI' ambapo alisema wanafanya mikutano kila mwezi kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi.

# Madiwani wahoji kutotengwa fedha ujenzi soko lililoungua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADIWANI wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya wamewabana wataalama wa Jiji hilo wakihoji hatua ya kutotenga fedha kwenye rasimu ya bajeti ya mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya Soko la Uhindini ambalo liliteketea kwa moto miaka 13 iliyopita.

Wamesema eneo hilo la Soko la Uhindini kwa sasa ni kama limetelekezwa kwa Wahindi ambao wameamua kulitumia kucheza gofu nyakati za jioni na siku za mapumziko bila kuingiza mapato yoyote kwenye halmashauri.

Diwani wa Kata ya Sisimba mahali lilipo soko hilo, Josephine Qamunga, alisema eneo hilo limebaki kuwa la wazi na linatumika na baadhi ya wananchi hasa wahindi kwa ajili ya kucheza mchezo wa gofu tofauti na malengo yake.

Alisema tangu soko hilo lilipoungua wananchi wamekuwa wakiahidiwa kuwa litajengwa upya na kuwa la kisasa lakini utekelezaji haupo na kwamba walitegemea kwenye bajeti ijayo ujenzi utafanyika.

"Nimeangalia kwenye vifungu vyote ikiwamo kwenye vipaumbele vyetu sijaona bajeti ya kujenga soko letu la Uhindini, kama inawezekana eneo hilo tuachieni tujenge hata shule maana inaonyesha soko limetushinda kabisa," alisema Josephine.

Alisema kenye bajeti na vipaumbele vya jiji hilo yametajwa masoko mengi isipokuwa hilo la uhindini ambalo ni miongoni mwa yaliyokuwa masoko makubwa ya jiji hilo.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, John Nchimbi alisema soko hilo ni moja kati ya miradi mikubwa ya jiji hilo ambayo inahitajika kutekelezwa kwa ushirikiano na wabia mbalimbali akidai kuwa wakitaka kutekeleza wao wenyewe inaweza ikachukua muda mrefu bila kukamilika.

Alisema wanaendelea na mazungumzo na baadhi ya wadau ikiwamo Benki ya Taifa ya Uwekezaji (TIDB) ambayo imeonyesha utayari kutekeleza mradi huo ambao alisema utakuwa miongoni mwa miradi ya kuupendezesha mji.

Alisema awali walikuwa na mazungumzo na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na walikuwa tayari kuutekeleza lakini baadaye wakabadilika baada ya uongozi wa juu kubadilishwa.

"Mimi binafsi nilishazungumza na Mkurugenzi wa Benki hiyo na Februari 28 mwaka huu Mstahiki Meya wetu na mchumi wamealikwa Dar es Salaam kwa ajili ya kwenda kufanya mazungumzo zaidi," alisema Nchimbi.

Alisema wanakusudia eneo hilo yatakuwapo maduka ya kisasa na benki mbalimbali na kwamba kitakuwa miongoni mwa vitega uchumi vitakavyokuwa vinavyoliingizia jiji fedha nyingi.

Meya wa Jiji la Mbeya, DorMohamed Issa aliwataka madiwani kuwa na subira wakati mipango ya kuwatafuta wawekezaji kwenye eneo hilo ambao watawekeza kwa tija na kuwa na manufaa makubwa kwenye halmashauri.

Alisema mbali na kumpata mwekezaji mwenye tija, pia wanahitaji eneo hilo lijengwe kisasa ili lipendeze na kuwa kivutio kwa wageni wanaoingia mkoani Mbeya.

Hivyo, aliwataka madiwani kuwaelimisha wananchi ili waelewe kinachoendelea kwenye eneo hilo pamoja na miradi mingine ya maendeleo ambayo inatekelezwa na serikali jijini humo.



# Wizara ya Afya yapongeza mfumo mpya ununuaji dawa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh amesema huduma ya tigo dawa ni mkombozi kwa wananchi visiwani hapa.

Amesema huduma hiyo itawawezesha wananchi kuwa na uhakika wa kupata dawa hata wanapokuwa hawana fedha wakati wa dharura.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo iliyoanzishwa na Kampuni ya Tigo na Laina Finance Limited, Naibu Waziri huyo alisema huduma hiyo ni mkombozi kwa wananchi wa Zanzibar.

Pia alizipongeza kampuni hizo kwa kuanzisha huduma hiyo itakayokuwa na msaada mkubwa kwa wananchi kuwezeshwa mtumiaji wa mtandao huo wa simu kupata huduma za dawa kwa njia ya mkopo na kurudisha fedha hizo kwa kipindi cha siku 10.

Hivyo aliwataka pia kubuni huduma nyingine mbalimbali ambazo zitaweza kuwasaidia wateja wao hasa katika kipindi cha dharura.

"Hii ni huduma ambayo itakuwa na msaada mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar ni wazi ugonjwa unakuja bila taarifa, kupata uhakika wa kupatiwa dawa ni Jambo la msingi sana, nawapongeza sana kwa huduma hii na niwaombe muangalie uwezekano wa kubuni kwenye malipo mengine," alisema Hafidhi.

Ofisa Mkuu wa Tigopesa, Angelica Pesha, alisema huduma mpya ya 'pata dawa' kutoka Tigo Pesa ni fursa mpya kutoka TigoZantel ambayo imehamasishwa na mfumo wa huduma za afya Zanzibar ambao unatoa huduma za matibabu bure kwa wananchi, huku ukihitaji wao kujikimu katika kununua dawa zao.

Alisema, kwa kutambua jitihada za serikali na uhitaji wa wananchi, Tigo Zantel imeshirikiana na Laina Finance, kuleta suluhisho ambalo litakidhi mahitaji ya wananchi wa Zanzibar na Tanzania Bara.

Alisema wataendelea kushirikiana na mamlaka za serikali kuhakikisha huduma hiyo inakuwa yenye tija mwa wananchi.

# Ombi la Dk. Mwinyi wajasiriamali kupewa gesi latekelezwa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

OMBI la Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi la wajasiriamali wanawake visiwani Unguja kupatiwa mitungi ya gesi, majiko ili kuwezeshwa kiuchumi pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa kutumia nishati safi ya kupikia limetekelezwa.

Akikabidhi mitungi ya gesi 1,000 iliyotolewa na kampuni ya gesi ya Orxy kwa wajasiriamali hao, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, alimshukuru Dk. Mwinyi kwa kutoa mapendekezo mahususi kwa kampuni ya Oryx gas kuwapa nyezo safi na salama wajasiriamali wanaofanya shughuli za kupika.

"Naomba mfahamu Rais Dk. Mwinyi alielekeza hili jambo katika dhana nzima ya kuweka urahisi kwa mjasiriamali mwanamke anapofanya shughuli zake katika jiko basi Oryx Gasi wasaidie katika kutoa nishati safi," alisema Soraga

Aliongeza: "Kwa hiyo tumpongeze Dk.Mwinyi kwanza kwa kuja na mawazo hayo, lakini kuthubutu kutoa maelekezo na leo hii tunakutana hapa kutoa mitungi ya gesi ambapo leo tukabidhi mitungi 1,000 kwa wajasiriamali wa Unguja na wiki chache zijazo itakabidhi mitungi mingine 1,000 kwa wajasiriamali wa wa Pemba."

Aliwashukuru kampuni hiyo akisema wamekuwa wadau muhimu katika sekta ya nishati Zanzibar hususani katika kufanikisha ajenda ya kutumia nishati mbadala katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.

Alisema Oryx kwa kipindi cha muda mfupi wamekuwa na kampeni endelevu ya kuhakikisha matumizi ya gesi safi na salama yanapewa kipaumbele sambamba na kumuunga mkono Rais Dk.Mwinyi katika malengo yake ambayo amekusudia kuifanya Zanzibar kuwa ni sehemu inayotumia gesi.

Naibu Waziri Soraga alisema serikali imekuwa na lengo la kuhakikisha inatoa fursa mbalimbali kwa wananchi ili waweze kumudu maisha.

Alisema kupitia mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi katika kipindi cha miaka mitatu kumekuwa na mafanikio makubwa na Sh.bilioni 27 zimetolewa katika kuwakopesha wananchi, wajasiriamali 26,000 wamenufaika. Naibu Waziri huyo alisema ni vema juhudi hizo ambazo wanashirikiana na wadau wakiwemo Orxy ziendelee na kubadilisha mtazamo wa namna ya kufanya shughuli.

Naibu Waziri huyo alisema kutumia nishati safi ya gesi kutamwezesha mtoto wa kike kujikita katika masomo na kazi nyingine za shuleni badala ya kutumia muda mwingi kutafuta kuni. Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania ltd, Benoit Araman alimshukuru Dk. Mwinyi kwa kuwaalika Zanzibar ili kufikisha nishati safi ya kupikia, huku akimpongeza kwa juhudi na kazi kubwa aliyoifanya kuhakikisha Zanzibar inakuwa sehemu kivutio kwa wawekezaji. Alisema: "Oryx ilianza kufanya biashara ya kupikia Zanzibar na Pemba mwaka 2016. Oryx Gas Zanzibar ilizinduliwa rasmi Desemba, 2021. Hii ni ishara ya kwanza ya imani katika utawala wake. Tangu kipindi hicho Dk. Mwinyi ametupa msukumo mkubwa wa kuendelea kuwekeza zaidi visiwani". Alisema wanajivunia kuchangia katika maendeleo ya muda mrefu visiwani Zanzibar, huku akitumia nafasi hiyo kueleza kupika kwa gesi kunasaidia kulinda mazingira na kutokomeza ukataji wa miti ili kutengeneza mkaa na kuni.

Alisema wamekabidhi mitungi ya gesi 1,000 kwa manufaa ya wananchi wa Unguja na hivi karibuni watakabidhi mitungi mingine 1,000 visiwani Pemba.




Msajili wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Waheed Ibrahim Sanya, akifungua kikao kazi na wakuu wa taasisi za uwekezaji za umma, mjini Unguja jana. **PICHA: MAELEZO ZNZ**

# Video ya mtoto akifanyiwa ukatili, serikali yachukua hatua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma amesema wizara yake imesikitishwa na kitendo cha ukatili wa kijinsia aliofanyiwa mtoto wa miaka 11 (jina limehifadhiwa), anaeishi Bububu visiwani Zanzibar.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisi kwake Kinazini Mjini Zanzibar, kufuatia video iliyokuwa ikisambaa katika mitandao ya kijamii ikimuonesha mtoto huyo akifanyiwa kitendo cha ukatili na mama yake wa kambo. "Wizara inalaani vikali tukio hilo, kwani kumfanyia ukatili wa aina yoyote mtoto ni kinyume na haki za mtoto kama inavyoelezwa katika Sheria ya Mtoto namba 6 ya Mwaka 2021 na hivyo ikibainika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake" alisema Riziki.

Hivyo aliwataka wananchi kuendelea kuwa na subira wakati vyombo vinavyohusika vikiendelea na uchunguzi juu ya tukio hilo.

Aidha alisema kutokana na tukio hilo, wizara imeamua kumuhifadhi mtoto huyo ili kupisha uchunguzi, kuwataka wananchi kuwa watulivu huku vyombo husika vikiendelea na taratibu zake. "Tunaiomba jamii kwa ujumla kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia vinamalizwa hapa nchini kwetu. Nitoe wito kwa wananchi kuripoti matukio au vitendo au viashiria vyote vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto. Serikali ipo kwa ajili yenu na itachukua hatua stahiki" alisema.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Riachard Mchomvu akizungumzia tukio hilo alisema Jeshi la Polisi linamshikilia mtuhumiwa wa tukio hilo na uchunguzi utakapokamilika atafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Kamanda huyo alisema mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo Febuari 11 akimdhalilisha mtoto huyo kwa kipigo kikali na kuwapongeza wasamaria wema waliochukua video wakati mama huyo akitenda kosa hilo na kuirusha katika mitandao ya kijamii.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**MWASA ELIA GASPARY** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba **TAE 612987,** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO tarehe 28 Julai 2023. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/20333/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SARAH .R. STEPHEN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1247-0128** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. MARKS SECONDARY SCHOOL** mwaka **2011.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/ILA/19131/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIHAIKA BRYCESON MATERU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0328/0020** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAWENZI SEKONDARI** mwaka **2002.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/5915/09.**

### THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT.
### (CAP 117)
### DEED POLL

**BY THIS DEED,** I the undersigned now and latterly called **PATRICIA SELESTIN MASERAGO DO HEREABY** absolutely renounces and abandon the use of my former names **PATRICIA MALEKELA KIMATA** as appeared in Public Service social security fund (PSSF) with registration No. 839069 and in lieu thereof do assume from the date hereof my name of **PATRICIA SELESTIN MASERAGO** as appeared in my National card with Entry No **19600812471020000119.** And in pursuance of such change of my names as aforesaid I **HEREBY DECLARE** that, I shall at all times hereafter in all records, deeds, instruction, instrument in writing in all actions and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of **PATRICIA SELESTIN MASERAGO** so renounced as aforesaid.

**AND I HEREBY** authorize and request all persons to designated and address me by such assumed name **PATRICIA SELESTIN MASERAGO** as appeared in my National Identity card with Entry **No 19600812471020000119**

**IN A WITNESS WHEREOF I** have hereunder signed my assumed name of **PATRICIA SELESTIN MASERAGO** and I have set my hand this 9 day of February, 2024.

Signed and Delivered at Kigoma

By the said **PATRICIA SELESTIN MASERAGO** who is introduced to me by..................................or who is personally known to me in my presesnce this 30 day of January, 2024.

Signed and Delivered at Kigoma
By the said PATRICIA SELESTIN MASERAGO who is
Introduced to me by ..............................or
Who is personally known to me in my presence
This 30 day of January, 2024

DEPONENT



BEFORE ME
Name:
Signature:
Address:
Commissioner for oath

### JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI ILIYOPO KATIKA WILAYA YA IRINGA

**SHAURI LA TALAKA TALAKA NO:05/2024**

**SAMSON MWIMO LAIZER.........................MDAI**

**DHIDI YA**

**SYLIVIA JOHN NYAKI ...........................MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

Mdaiwa Sylivia John Nyaki popote pale ulipo unatakiwa kufika Mahakamani Terehe 27/02/2024 saa2:30 asubuhi kwajili ya shauri la Talaka.

Usipofika tarehe husika Shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 13/02/2024.

Hakimu Mahakama ya Mwanzo.
IRINGA MJINI
RESIDENT MAGISTRATE IRINGA

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICES LTD, SEPCO DEBT COLLECTION & AUCTIONEERING CO LTD** tunautangazia umma kuwa kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza mali ya mdaiwa kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdaiwa | Dalali | Aina ya Mali /Mahali | Tarehe mnada |
|---|---|---|---|
| Vicent Ringson Mberesero | SEPCO Debt Collection & Auctioneering CO. LTD | Mitsubishi Canter T.682 DUC, Makumbusho Yard- Dar | 22 Feb 2024 |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.

Gharama za kukagua na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: -**
**SEPCO:- 0715683777/0716535221**

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya Bukoba**
**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa wa Kagera,**
**Shauri la Madai Na. 22/2024**
**Jina la Mdai.............. Musa Tito Nuhu**
**Jina la Mdaiwa ........Kyanala Investment Co. Ltd (Zakaria Mwaipopo)**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Kwa Kyanala Investment Co. Ltd (Zakaria Mwaipopo)**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/ wameleta madai yake/yao ya shilingi 7,500,000, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 27 Mwezi 2 Mwaka 2024 saa 8:00 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 12 Mwezi 2 Mwaka 2024.

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA BUKOBA MJINI
HAKIMU

### KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
### WILAYA YA KINONDONI
### MWANANYAMALA

**SHAURI LAMADAI NAMBARI...594...LA .....2023**
**MWINYIMKUU SELEMANI......MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MICHAEL MTWEVE............MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**MICHAEL MTWEVE**
**POPOTE ULIPO/MLIPO:**
**MWINYIMKUU SELEMANI** Amefunga shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 19/02/2024 ..........Asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 30 Mwezi 01 ......2024


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa Tupigie +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wanawake wasimulia machungu wanayoyapitia Gaza

**GAZA,** PALESTINA

VITA vinavyoendelea katika Ukanda wa Gaza mbali na kusababisha madhara mbalimbali ikiwamo kugharimu maisha ya watu, kusababisha vilema na kuharibu miundominu ya kijamii, imesababisha wanawake na watoto kugeuka wakimbizi wanaotanga tanga huku na kule kusaka hifadhi.

Akizungumza wakati wa mahojiano aliyofanyiwa na CNN jana Walla Al-Arbeel, ambaye ni miongoni mwa wahanga, alisema kuwa wakiwa katika jengo moja walilolitumia kama maficho, wanajeshi wa Israel walikuja na kuwazingira kwa mizinga na kushindwa kutoka nje, wala kuwasha taa kwa kuhofia kuonekana na kwamba hawakuwa na chakula wala maji.

Alisema dada yake, ambaye ni daktari, kaka wawili na mumewe walichukuliwa, na kwamba hajui kilichowapata.

"Baada ya kufanikiwa kuondoka kwenye jengo hilo, wanajeshi wa Israel hawakuniruhusu ninywe maziwa kwa ajili ya mwanangu. Hakuna koti kwa watoto wangu. Walikuwa peku. Hakuna kitu, nilikuwa nikiwaomba, lakini hawakunipa chochote," alisema.

Akielezea safari ya kwenda hospitalini, alisema hawakuwa na chakula wakati wakizingirwa na kwamba watoto waliendelea kuomba chakula ... kipande cha mkate na maji bila mafanikio.

Alieleza kuwa wakati wa kutembea kwa muda mrefu kwenye fukwe kwenye mvua ya baridi, aliogopa kuwa mbwa waliopotea walikuwa wakiwawinda watoto, na wakati mmoja mama yake wa kambo alianguka na kushindwa kutembea katika eneo ambalo halikuwa salama.

"Aligeuka kuwa bluu, alichoka sana ... nilijaribu, nilitaka kumsaidia na kumletea msaada, lakini sikuweza, nilimlilia sana, niliendelea kumwambia, simama, jaribu tu kutembea, inuka, aliniambia niache tu, nenda tu kutoka kwa Waisraeli. aliendelea kusema, nenda, nenda, nenda, sitaki wakupige risasi," alisema.

"Nilimfunika, sikuweza kufanya chochote kwa ajili yake, mbwa walikuwa karibu naye ... nilimwacha hai, nikampa chupa ya maji na kumwambia anisamehe kwamba singeweza kumsaidia," alisema.

Binti aliyejitambulisha kwa jina la Harb Tala (10), alieleza kuwa wanajeshi wa Israel waliwalazimisha kuondoka katika jengo walilokuwa wamejificha, huku wakiwachukua ndugu zake.

"Walimchukua baba yangu, mjomba na binamu zangu, wakawaamrisha wavue nguo zao zote, Baba yangu ni mgonjwa na anaweza kufa kutokana na baridi... Hata mjomba na babu yangu waliwaacha na nguo zao za ndani na shati la mikono mifupi," alisema.

Tala alisema aliogopa kwamba Waisraeli wanaweza kulipua jengo hilo huku wanaume wa familia hiyo wakiwa bado ndani, lakini hakujua kwa uhakika ni nini kilikuwa kimewapata.

Mwanachama mwingine wa familia hiyo, Warda El Helw, pia alikumbuka mama wa kambo wa Harb alianguka wakati wa safari. "Hatukuweza kumsaidia; hakuweza kuendelea na akaanguka ufukweni. Alituambia tumuache na tuende, na kwamba Mungu yuko pamoja naye, kwa hiyo tukamfunika na kuondoka," alisema.

"Tulikuwa tukitembea ndani ya maji, juu ya mchanga na matope, maji taka na mawe kwenye miguu yetu," alisema.

**UN**

Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kibinadamu Volker Türk, alisema majeshi ya Israel yanatekeleza ubomoaji wa majengo ya makazi na majengo mengine ya kiraia katika eneo lote la kitongoji, ikiwa ni pamoja na katika mji wa Gaza.

Ilielezwa kuwa kitongoji cha juu cha Al-Rimal katika Mji wa Gaza kimeharibiwa na kampeni kali ya Israel ya kulipua mabomu, iliyozinduliwa kujibu mashambulizi mabaya ya Hamas nchini Israel mnamo Oktoba 7, 2023.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya inayoongozwa na Hamas huko Gaza hadi sasa zaidi ya Wapalestina 28,000 wameuawa na 66,000 kujeruhiwa katika mashambulizi ya Israel tangu vita kuanza.

**KAULI YA ISRAEL**

Jeshi la Israel (IDF) lilipoulizwa juu ya tuhuma hizo walisema kuwa vikosi vya taifa hilo vilikuwa vikifanya kazi katika ngome za Hamas kama sehemu ya juhudi zao za kusambaratisha uwezo wa kijeshi wa kundi hilo na kuwaokoa mateka wa Israel waliotekwa na Hamas.

"Katika hali ambayo askari wanashindwa kuzingatia maagizo ya IDF, matukio yanakaguliwa kwa kina, na hatua za kinidhamu hutekelezwa, ikiwa ni lazima," ilisema IDF.

**CNN**



Muonekano wa makazi ya wananchi wa Gaza baada ya kushambuliwa na makombora ya Jeshi la Israel. **PICHA MTANDAO.**

# Waziri wa ulinzi Liberia ajiuzulu

**MONROVIA,** LIBERIA

WAZIRI mpya wa Ulinzi wa Liberia, Prince Johnson amejiuzulu wadhifa wake ikiwa ni siku 10 tu baada ya kuteuliwa, kwa kile kinachotajwa kuwa ni kwasababu ya maandamano yaliyofanywa na wake wa wanajeshi wa nchini humo.

Katika taarifa iliyotolewa na ofisi ya Rais wa nchi hiyo Joseph Boakai, jana alisema amepokea na kukubali barua ya kujiuzulu waziri huyo.

"Katika barua yake, Johnson ametaja machafuko ya sasa ya kisiasa na ya kiraia yaliyosababisha maandamano kuwa ni sababu ya kujiuzulu kwake, na ameeleza kuwa amefanya hivyo ili kulinda amani na usalama wa nchi," alisema.

Ilielezwa kuwa wanawake hao walioandamana waliweka vizuizi barabarani ikiwemo karibu na mji mkuu Monrovia, huku wakimtaka Rais Boakai kuboresha masuala kadhaa ikiwemo mishahara ya wanajeshi, na huduma za kijamii.

Rais Boakai ambaye maandamano hayo ni changamoto ya kwanza iliyomkuta tangu aingie madarakani, alitoa wito kwa wananchi kuwa watulivu huku akiahidi kuwa serikali yake itashughulikia matatizo yao. **DW**

# Afrika Kusini kupeleka wanajeshi 2,900 DRC

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa amesema nchi yake itatuma wanajeshi 2,900, kama sehemu ya mchango wake kwa kikosi cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kinachotarajiwa kukabiliana na makundi yenye silaha mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Katika taarifa aliyoitoa jana alisema kuwa operesheni hiyo ya mwaka mmoja ni ya kati ya Desemba 15, mwaka 2023 na Desemba 15, mwaka huu, na itagharimu takriban dola za Marekani milioni 105.75, zaidi ya Sh bilioni 267.

SADC, yenye nchi wanachama 16, iliidhinisha vikosi kutumwa mashariki mwa Congo mwezi Mei 2023, kusaidia nchi hiyo, msambazaji mkuu wa cobalt duniani na mzalishaji mkuu wa shaba barani Afrika, kukabiliana na hali ya kukosekana kwa utulivu na kuzorota kwa usalama katika eneo la mashariki.

Miongo kadhaa ya migogoro mashariki mwa DRC, kati ya makundi hasimu yenye silaha, yakizozania ardhi na rasilimali, imepelekea vifo vya mamia na maelfu ya watu na kusababisha zaidi ya watu milioni saba kukimbia makazi yao.

Kikosi cha SADC kinajumuisha wanajeshi kutoka Malawi, Afrika Kusini na Tanzania. Na kwamba kutumwa huko kunajiri wakati Congo inapambana na waasi wa M23 wanaoongozwa na Watutsi, ambao mashambulizi yao katika siku za hivi karibuni, yanatishia mji mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini, Goma.

**VOA**




Moses Ntilema akionesha tuzo na medali mbalimbali alizoshinda kwenye michezo ya uokoaji majini kati ya mwaka 2017 na 2019. **PICHA: MAKTABA**

# NTILEMA ATOA KILIO BMT UWAKILISHI MICHEZO YA UOKOAJI MAJINI AFRIKA

**Na Mwandishi Wetu**

MTANZANIA anayeishi Afrika Kusini, Moses Ntilema, ambaye ni mtaalamu wa usalama na uokoaji majini pia mwanamichezo wa michezo ya uokoaji majini, amepaza sauti yake kwa Baraza la Michezo nchini (BMT), akilitaka kumpa nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye International Lifesaving Federation African Championship 2024, yatakayofanyika kuanzia Machi 18-20, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu kutoka Afrika Kusini, Ntilema alisema alishaimboa BMT kumapa nafasi hiyo ya kuiwakilisha nchi lakini katika mashindano hayo lakini bado hajapata mrejesho, hivyo ameona ni vema tena akatoa kilio chake hicho.

"Kwa mara kadhaa nishaongea na baadhi ya viongozi wa vyombo husika nchini hasa kupitia WhatsApp na barua pepe kuhusu utayari wangu wa kushiriki mashindano hayo.

"Na kama ni gharama kwao, basi niko tayari kujigharamia kambi ya mazoezi, usafiri na vifaa ili kushiriki mashindano hayo muhimu. Ninachohitaji sana ni taasisi husika yaani Tanzania Lifesaving Society kusajili jina langu katika mashindano hayo. Naamini kuwa mimi Moses Ntilema ni miongoni mwa Watanzania wachache wenye uwezo mzuri katika Michezo ya uokoaji baharini yaani 'Surf Lifesaving Sports'," alisema na kuongeza;

> **"Ninaumia sana kuona wadau wa Lifesaving duniani wakiniuliza kwa nini siiwakilishi Tanzania wakati uwezo ninao na nimekuwa nikionekana nafanya vema kwenye ngazi za klabu."**

Ntilema alisema mwaka 2018, 2019, na 2021alishiriki mashindano ya South Africa National Lifesaving Championship na kushinda medali kadhaa, jambo ambalo anaamini anaweza kuitangaza vema Tanzania kwa kuiletea medali kwenye michuano hiyo.

"Tukumbuke kuwa kushiriki na kushinda medali si jambo rahisi kwani Afrika ya Kusini inaongoza barani Afrika kwa michezo ya uokoaji majini pia ni miongoni wa nchi tano duniani zilizoanzisha International Lifesaving Federation, hivyo hutoa upizani mkubwa na mataifa mengine duniani kwenye michezo ya majini.

Alisema: "'Si lazima nishinde bali kujipima kabla ya kushiriki mashindano ya dunia Agosti mwaka huu huko Australia, pia kuitumia fursa hii pekee kuitangaza Tanzania kuhusu utalii wa fukwe hasa Zanzibar."

Alisema bado ana matumaini BMT inaweza kulishughulikia na ndio maana amerudi tena kwao kabla ya kubisha hodi kwa wizara husika ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

# Chipukizi yawahofia waburuza mkia Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa 18 ikiendelea leo kwa kupigwa mchezo mmoja katika dimba la Mau A Kisiwani hapa, timu ya Chipukizi FC imewahofia wapinzani wao, Ngome FC licha ya kwamba wanaburuza mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Ngome FC inashuka dimbani ikiwa inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu lakini pia ikiwa na kumbukumbu mbaya ya kupoteza michezo yote miwili ya mzunguko huu wa pili wakati Chipukizi FC wakipoteza mmoja na kushinda mmoja.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu ya Chipukizi FC, Mzee Ali Abdalla, alisema mchezo huo ni muhimu kwao kupata alama tatu ili kujiweka sawa katika msimamo wa ligi hiyo.

Alisema wanaenda kucheza na timu ambayo haikupata matokeo katika michezo miwili mfululizo, lakini pia ipo katika mstari wa hatari wa kushuka daraja, hivyo lazima wawe makini.

Kocha huyo alisema wapinzani wao watakuja na mbinu ya kushambulia ili kuhakikisha wanashinda mchezo huo, hivyo kama mwalimu, anatakiwa kuwasoma wapinzani wake katila dakika za mwanzo za mchezo.

Alisema licha ya kila timu kutaka kutamba katika uwanja wa nyumbani, lakini katika mzunguko wa lala salama huwa mgumu zaidi bila kujali kama upo nyumbani au ugenini.

"Tumejipanga kukabiliana na mzunguko huu muhimu sana, lengo letu ni kuhakikisha tunamaliza ligi tukiwa katika nafasi za juu kwenye msimamo, hivyo lazima wachezaji waendelee kujituma kama ilivyo katika michezo iliyopita, bila ya kudharau tunacheza na timu ipi," alisema.

Alisema kuelekea mchezo huo kikosi chake kimejiandaa kutoa burudani ya nguvu, hivyo wanawaomba mashabiki wa timu hiyo waliopo Unguja kujitokeza kwa wingi uwanjani ili kuipa hamasa timu yao.

Chipukizi FC ipo nafasi ya nane ikiwa na alama 22 wakati wa pinzani wao wanaburuza mkia wakiwa na pointi 12.

# Nyumbu FC, Mapinduzi vinara Ligi Daraja la Pili

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Nyumbu ya Pwani, juzi ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Dar City na kukwea juu ya msimamo wa Ligi Daraja la Pili Ngazi ya Taifa 'First League', Kundi A, mechi ikichezwa Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Wakati Nyumbu ikiongoza kundi hilo, timu ya Mapinduzi nayo imeichapa Mwadui FC mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Geita na kuliongoza Kundi B.

Ligi hiyo inaendelea kwenye viwanja mbalimbali nchini kusaka timu zitakazopanda Ligi ya Championship msimu ujao.

Nyumbu ipo kileleni ikiwa na pointi 16, ikicheza mechi nane, ikishinda tano, sare moja, ikipoteza mbili.

Hata hivyo, inafuatiwa kwa karibu na Kiluvya yenye pointi 15, African Sports nafasi ya tatu na pointi 14, Malimao FC nafasi ya nne ikiwa na pointi 13, Tunduru FC iko katika nafasi ya tano na pointi zake nane, Dar City ya sita ikiwa na pointi sita, African Lyon ya saba pointi zake nne na Lipuli ikiwa inashikilia mkia.

Kundi B ambalo linaongozwa na Mapinduzi FC, ambayo ina pointi 20 kwa mechi nane ambazo imecheza na inafuatiwa mbali kidogo na Tanesco FC, yenye pointi 16.

TRA FC, ipo kwenye nafasi ya tatu ikiwa na pointi 15, Rhino Rangers ya nne ikiwa na pointi 15 pia, Mwadui FC ya tano na pointi zake 10, Alliance FC inashika nafasi ya sita na pointi zake tano, Kurugenzi FC ya saba ina pointi nne na Kasulu United inaburuza mkia ikiwa na pointi moja tu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**SILVA AWANIWA PSG**

KIUNGO wa kati wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 29, anawaniwa na Paris St-Germain, huku mabingwa hao wa Ufaransa wakiwa tayari kulipa dau lake la pauni milioni 51. (*Fichajes*)

**ANGE KUBAKI SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur ina imani kuwa kocha, Ange Postecoglou mwenye umri wa miaka 58, atabaki katika klabu hiyo licha ya Liverpool kumtaka huku 'Wekundu' hao wakitafuta atakayechukua mikoba ya Jurgen Klopp msimu huu wa majira ya joto. (*Telegraph*)

**MOYES ACHELEWESHWA**

KLABU ya West Ham imechelewesha mazungumzo ya mkataba mpya na kocha, David Moyes mwenye umri wa miaka 60, huku klabu hiyo ikilenga kumaliza mfululizo wa mechi saba bila kushinda katika michuano yote. (*Mail*)

**DE LIGT AIVUTIA UNITED**

MANCHESTER United inavutiwa na mlinzi wa Bayern Munich, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 24, ingawa mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uholanzi hajafurahishwa na nafasi yake katika kikosi cha mabingwa hao wa Ujerumani. (*Sun*)

**ARSENAL NAO KWA DE LIGT**

ARSENAL pia wanania ya kumnunua Matthijs de Ligt, lakini Manchester United kwa sasa wako katika nafasi nzuri. (*Football Transfers*)

**MABEKI WATAKIWA UNITED**

MABEKI wawili wa Bayer Leverkusen pia wanafuatiliwa na Manchester United, huku kocha wa 'Mashetani Wekundu' hao, Erik ten Hag, akimtaka beki wa kulia wa Uholanzi, Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 23, na mlinzi wa kati wa Burkino Faso, Edmond Tapsoba, 25. (*Manchester Evening News*)

**ARSENAL, LIVER KWA NETO**

KLABU za Arsenal na Liverpool zina nia ya kumsajili winga wa Ureno, Pedro Neto kutoka Wolves, ambao wako tayari kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ikiwa thamani yao itafikiwa kwa sababu ya shinikizo la kifedha linaloendelea. (*Fichajes*)

**KERKEZ AFUATILIWA**

CHELSEA inamfuatilia beki wa kushoto wa Bournemouth na Hungary, Milos Kerkez mwenye umri wa miaka 20, pamoja na beki wa pembeni wa Bayern Munich na Canada, Alphonso Davies, 23. (*Football Transfers*)

**FULHAM NA HALLER**

KLABU ya Fulham ilishindwa katika jaribio la kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Sebastien Haller, Januari huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, akitaka kuelekeza nguvu zake kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika akiwa na Ivory Coast na hakutaka kuhama katikati ya msimu. (*Fabrizio Romano*)

**BARCA KUUZA NYOTA**

BARCELONA imewaweka sokoni beki wa Denmark, Andreas Christensen na winga wa Brazil, Raphinha, wote wakiwa na umri wa miaka 27, katika oodha ya wachezaji wanaopangwa kuuzwa ili kupunguza bili yao ya mishahara. (*Mirror*)

**ALONSO LULU SOKONI**

KOCHA wa Bayern Leverkusen, Xabi Alonso sasa anasakwa na Barcelona pamoja na Real Madrid na Liverpool. (*Sport*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE HAELEWEKI KUHUSU HATIMA YAKE

**PARIS,** Ufaransa

**Hivi karibuni alinukuliwa akisema anataka kucheza na wachezaji bora, lakini...**

KYLIAN Mbappe bado hajaeleza nia yake ya kuondoka Paris Saint-Gemain au kujiunga na Real Madrid msimu huu wa majira ya joto, kwa mujibu wa ripoti.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa, kwa muda mrefu amekuwa akionekana kudhamiria kuhamia kule Bernabeu na yuko katika miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na wababe wa Ufaransa, PSG.

**90min iliripoti Januari kwamba Mbappe lazima amjulishe rais wa Klabu, Nasser Al-Khelaifi kwanza mara tu atakapoamua ni wapi uti wake wa siku zijazo upo.**

Kambi yake hadi sasa imesisitiza hakuna makubaliano yoyote yaliyofikiwa na 'Los Blancos' juu ya makubaliano ya baadaye.

Gazeti la The Athletic linaelewa Mbappe bado hajatoa neno lake kwa PSG au Madrid, huku baadhi ya wapambe wake wakisemekana 'hawajashawishika' kuhusu ofa hiyo kutoka Hispania.

Ripoti yao inaongeza kuwa bosi wa Real Madrid, Florentino Perez, amekuwa akiwasiliana mara kwa mara na Mbappe na akajiondoa ili kuhakikisha dili linaweza kufungwa.

Fedha za dili hilo hazina faida kubwa kwa Mbappe kuliko ambavyo ingekuwa kama mazungumzo yangekamilika mwaka 2022.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, bado anaweza kuwa mchezaji anayelipwa vizuri zaidi kwenye kikosi cha Carlo Ancelotti.

Mbappe alikiri Januari kwamba atalazimika kuondoka Ligue 1 "wakati fulani", baada ya kuwa mfungaji bora wa PSG na mfungaji bora wa tisa katika historia ya Ligi Kuu Ufaransa.

Mabingwa hao wa Ufaransa tayari wanajiandaa kwa kuondoka kwake.

Kikosi hicho cha kocha, Luis Enrique kimeandaa orodha fupi ya wachezaji wanaoweza kuchukua nafasi hiyo iwapo ataondoka, huku Marcus Rashford na Victor Osimhen wakizingatiwa kama mbadala wa majina makubwa.

Winga wa Madrid Rodrygo hivi majuzi alizungumzia furaha yake katika kuunganishwa na Mbappe katika mji mkuu wa Hispania, akikiri: "Nataka kucheza na wachezaji bora."

Pande zote mbili ziko kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki hii.




# REAL MADRID IMEJIZATITI BILA BELLINGHAM – ANCELOTTI

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amesema timu yake ya Real Madrid imejiandaa bila ya uwapo wa Jude Bellingham ambaye ni majeruhi, baada ya nyota huyo kuteguka kifundo cha mguu mwishoni mwa wiki.

Bellingham aliumia katika dakika ya 57 ya ushindi wa mabao 4-0 wa LaLiga Jumamosi dhidi ya Girona - matokeo ambayo yaliiweka Madrid kwa pointi tano kileleni mwa jedwali la ligi - na vyanzo viliiambia ESPN kuwa mchezaji huyo wa Kimataifa wa England alitarajiwa kuwa nje ya dimba kwa wiki tatu.

Bellingham ndiye mfungaji bora wa Madrid msimu huu akiwa amefunga mabao 20 katika michuano yote, yakiwamo manne kati ya mechi tano za Ligi ya Mabingwa Ulaya hadi sasa na miamba hao wa LaLiga wakiongoza kundi lao.

"Hatufikirii kamwe kuhusu wale wachezaji ambao hawapo hapa," alisema Ancelotti katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mechi ya jana Jumanne dhidi ya Leipzig.

"Ni haki zaidi kufikiria waliopo hapa. Bila Bellingham, tumeshinda michezo minne kati ya minne msimu huu. Wale waliochukua nafasi yake wamefanya vema, iwe ni Brahim Diaz au Joselu.

"Bellingham ni mchezaji mzuri sana - kama Thibaut Courtois, Eder Militao, David Alaba - lakini kesho ni fursa ya kuwa na motisha zaidi."

Wakati huo huo, Kiungo wa kati wa Madrid, Toni Kroos, alisema bado hajaamua kama ataongeza mkataba wake na klabu hiyo zaidi ya msimu huu wa majira ya joto, na kama kurejea kwa mshangao katika Timu ya Taifa ya Ujerumani kwa ajili ya michuano ya Euro, baada ya kustaafu mwaka 2021.

"Siku zote huwa nakuambia ukweli, na ukweli ni kwamba sijui," alisema Kroos.

"Ninafikiria juu ya kile ninachotaka kufanya. Sijaamua chochote bado. Inanifurahisha kwamba watu wanataka nicheze mwaka mmoja zaidi, hiyo ni bora kuliko njia nyingine kote, wakitaka niache!"

Kroos, ambaye ameichezea Madrid msimu huu, aliichezea Ujerumani mechi 106, akishinda Kombe la Dunia 2014, kabla ya kustaafu baada ya Euro 2020.

"Inategemea mambo mengi," alisema Kroos alisema.

"Nataka kumalizia soka langu kwa kiwango cha juu zaidi. Ninafurahia wakati huu. Ninastahili muda zaidi kuchukua uamuzi, nataka uwe sahihi...na vivyo hivyo kwa timu ya taifa. Ninafikiria juu yake, lakini kama vile nilivyofanya upya, sijui."

# Kocha Ivory Coast bado haamini



**ABIDJAN,** Ivory Coast

KOCHA wa muda wa Ivory Coast, Emerse Fae, hakuweza kuelezea hisia zake kuu za kuwaongoza Tembo hao kubeba ubingwa wa Kombe la mataifa ya Afrika, Afcon, nyumbani.

Fae amesema kuwa bado haamini kama kweli yeye ameiongoza Ivory Coast kubeba kombe hilo kwa mara yao ya tatu katika historia.

Ivory Coast ilitoka nyuma na kufanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Nigeria kwenye Uwanja wa Alassane Ouattara mjini Abidjan Jumapili jioni.

Akizungumza wakati huu wakiendelea na sherehe za ubingwa huo, Fae ambaye alichukua nafasi ya Kocha Mkuu, Jean-Louis Gasset, alisema ni ngumu kuamini kwamba, walikaribia kutolewa na sasa wameshinda taji hilo.

"Bado naona vigumu kuamini. Tulipitia hisia zote. Ushindani huu utaashiria maisha yangu, hiyo ni hakika.

"Nilichukua mikoba ya timu tena wakati wa siku yangu ya kuzaliwa na nusura tutupwe nje, lakini mambo yaligeuka kutokana na bidii ya wachezaji hawa na sasa wamezawadiwa na kikubwa zaidi wametuza watu wetu waaminifu," alisema kocha huyo.

Fae pia alitwaa tuzo ya Kocha Bora wa Mashindano kwa kuonesha ustadi wa kuwaongoza 'Tembo' hao hadi kubeba kombe.

# Mlango uko wazi Messi kucheza Olimpiki

**BUENOS AIRES,** Argentina

LIONEL Messi ana mwaliko wa wazi wa kucheza katika kikosi cha Argentina cha Olimpiki msimu huu wa majira ya joto, kwa mujibu wa kocha, Javier Mascherano.

Argentina waliwashinda washindi wa medali za dhahabu, Brazil kwa bao 1-0 na kujihakikishia nafasi ya kushiriki michezo ya Olimpiki huko Paris nchini Ufaransa baadaye mwaka huu.

"Kila mtu tayari anajua uhusiano wangu na Leo Messi, urafiki nilionao," alisema Mascherano.

"Mchezaji kama yeye ana milango wazi ya kutusindikiza kwenye Olimpiki, basi itategemea yeye na ahadi zake."

Messi, ambaye aliiongoza nchi yake kunyakua taji lao la tatu la Kombe la Dunia mwaka 2022, alisherehekea Argentina kufuzu kwa Olimpiki kwa kutuma kwenye Instagram picha ya timu ya Mascherano baada ya ushindi wa Jumapili.

Kiungo wa Argentina chini ya umri wa miaka 23, Thiago Almada alisema itakuwa ndoto kuwa na mshindi wa Ballon d'Or mara nane Messi kwenye kikosi cha Olimpiki.

"Natumani ana nia, kwamba anaweza kuwa huko," alisema Almada anayeichezea Atlanta United.

"Lazima tuone jinsi alivyo wakati huo, itakuwa ndoto kwamba angeweza kucheza."

Messi alishinda medali ya dhahabu katika michezo ya Olimpiki mjini Beijing mwaka 2008 na rais wa Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki, Thomas Bach hivi majuzi alisema itakuwa "nzuri sana kwa michezo ya Olimpiki kumrejesha."

Hata hivyo, Messi tayari ameeleza nia yake ya kutaka kushiriki michuano ya Copa America 2024 itakayoandaliwa nchini Marekani kuanzia Juni 20 hadi Julai 14, chini ya wiki mbili kabla ya michezo hiyo kuanza jijini Paris.



HABARI MICHEZO

# AJIB AKUNWA KIWANGO COASTAL

**Na Saada Akida**

LICHA ya kutoka suluhu dhidi ya wenyeji wao, KMC FC, kiungo mshambuliaji wa Coastal Union, Ibrahim Ajib, ameeleza kufurahishwa na maendelea ya timu yao hususan uwezo wa kutengeneza nafasi nyingi, jambo ambalo sasa wanatakiwa kuongeza umakini wa kuzitumia katika mechi zijazo.

Amesema awali katika mechi nyingi zilizopita hawakuwa wakitengeneza nafasi nyingi kama ilivyo kwa mchezo huo wa mzunguko wa pili, hivyo ana imani katika michezo inayofuata kama wakiendelea kutengeneza, watazitumia ipasavyo.

Akizungumza na Nipashe baada ya kukamilika kwa dakika 90 za mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC, Ajib alisema mechi ilikuwa mzuri na kukosa umakini wa safu ya ushambuliaji kuliwanyima mabao.

Alisema walikuja Dar es Salaam kutafuta pointi tatu, lakini wamevuna alama moja, na kwamba si haba, hivyo sasa wanasahau matokeo ya mechi hiyo na kuangalia iliyokuwa mbele yao.

"Ni kweli huu ni mchezo wetu wa kwanza kwenye duru la pili, tulikuwa kwenye mapumziko mafupi ambayo tuliyatumia kusahihisha makosa yetu ya mechi zilizopita, ni jambo la kumshukuru Mungu tumetengeneza nafasi nyingi katika mcheso huu dhidi ya KMC FC.

"Suala la kutengeneza nafasi ni kubwa sana kwetu na kufunga hilo ni jambo lingine, ninaimani benchi la ufundi limeona makosa hayo na watayafanyia kazi," alisema Ajib.

Alisema wanasahau matokeo hayo na kurejea Tanga, kujiandaa na mchezo ujao dhidi ya Dodoma jiji FC kuhakikisha wanawafurahisha Wanatanga kwa kuvuna pointi tatu katika uwanja wa nyumbani.



**SIKUBALI...** Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, akijaribu kufunga kwa kichwa lakini Kipa wa Geita Gold FC, Costantine Malimi, akawa makini kuucheza mpira katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza na Simba kushinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Gamondi aishtukia Simba, ageukia beki

INATOKA UK 24

kazi mapema kwenye safu yake ya ulinzi.

Alisema licha ya kupata ushindi, wamekuwa wakiruhusu nyavu zao kutikiswa jambo ambalo anaamini hapo baadaye litakuja kuathiri kwani wanaweza kupoteza au kupata sare kwenye moja ya mechi, ikawa ni hatari katika mbio zao za ubingwa kwa kuwa Simba inaonekana kuwa ya moto hivi sasa tofauti na ile aliyokuwa akiiona awali.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa, timu zimefanya maboresho makubwa, tunatakiwa kujiandaa vizuri katika michezo yetu ijayo kuhakikisha tunafanikiwa kuvuna alama tatu, lakini tusiruhusu nyavu zetu kutikiswa.

"Inapotokea mpinzani anaanza kupata bao la mapema kabla yetu na wengi wao hupenda kupoteza muda, itakuwa ngumu, tunatakiwa kulifanyia kazi jambo hilo mapema kwa safu ya ulinzi kuongeza umakini," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa anahitaji kufanya maboresho hayo mapema zaidi kwa kusahihisha kuanzia safu ya ulinzi akiamini nafasi ya ushambuliaji haina tatizo kubwa kwa sababu viungo na mawinga hufanya jukumu hilo la kufunga.

Gamondi alisema mechi ijayo wanarudiana na KMC FC mzunguko wa pili, ambapo ya raundi ya kwanza walishinda 5-0, lakini anaamini watabadilika na kuja kivingine hali ambayo analazimika kuandaa kikosi chake vizuri.

Yanga itawakaribisha KMC FC ukiwa mchezo wa mzunguko wa pili wa ligi hiyo utakaochezwa Jumamosi katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

# Wachezaji Mtibwa Sugar watupiwa lawama kukubali kipigo Ihefu

**Na Adam Fungamwango**

KIPIGO cha mabao 3-2 ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani, Manungu Complex, Turiani Morogoro, juzi dhidi ya Ihefu, kimemuibua Ofisa Habari mkongwe wa timu ya Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, akisema wachezaji wa timu hiyo wanastahili kubeba lawama.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kutamatika, Kifaru alisema wachezaji wa Mtibwa hawakutumia nafasi nyingi walizozipata kwani walikuwa wakishikwa na kigugumizi cha miguu wanapobaki na kipa.

"Wachezaji wetu wanastahili kubeba lawama, walilikaribia mara kadhaa lango la wapinzani kuliko hata wapinzani wetu, walikuwa na kigugumizi wanapofika langoni, kutokuwa na umakini, wenzetu waliweza kupata nafasi chache wakazitumia vema," alisema Kifaru.

Alisema pamoja na kukosa mabao, lakini walicheza vema huku ikiwa na wachezaji wengi wapya waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo ambao bado hawajazoeana

"Pamoja na hayo bado wachezaji wetu walicheza vema, Ihefu ni timu nzuri sana waliweza kutumia mapungufu yetu kutuadhibu, matokeo haya yanatuumiza sana, najua tutakaa vizuri, wachezaji wetu tuliowasajili kipindi cha dirisha dogo wakizoeana na wenzao timu itakaa sawa," alisema.

Baada ya kipigo hicho, Mtibwa imemaliza mechi zake za mzunguko wa kwanza ikikamata mkia kwa kuambulia pointi nane tu, katika michezo 15 iliyocheza mpaka sasa, ikishinda mechi mbili, sare mbili, ikipoteza mechi 11.

Katika mechi hiyo, mabao ya Ihefu yalifungwa na Duke Abuya, Marouf Tchakei na Elvis Rupia, ya Mtibwa yakiwekwa wavuni na Kassim Shaaban na Juma Lazio.

# *Kilio Simba chasikika, Kayoko kikaangoni*

INATOKA UK 24

Mbali na mechi hiyo, kumekuwa pia na malalamiko ya maamuzi tata kwenye mechi kadhaa za Ligi Kuu hivi karibuni hasa baada ya urejeo uliotokana na mapumziko ya Kombe la Mapinduzi na Fainali za Mataifa ya Afrika, AFCON.

Wakati huo huo, Kocha Daniel Cadena ameapa kuhakikisha wanacheza kwa ajili ya kuchukua pointi tatu na si vinginevyo.

Juzi, Simba ilipata ushindi wa bao 1-0 lililofungwa na Babakar Sarr dakika tisa kabla ya mechi kumalizika dhidi ya Geita Gold, Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kocha huyo alisema kwa sasa hawahitaji mambo mengi, bali kuhitaji ushindi ili kuweza kuufukuzia ubingwa.

"Tumecheza kwenye uwanja ambao kiukweli si rafiki na tulijua hivyo, kwa hiyo tulicheza kwa ajili ya kutafuta matokeo na si vinginevyo.

"Tumecheza mechi mfululizo pia, kumbuka kati ya siku 10 tu tumeshacheza mechi tano, nne za Ligi Kuu na moja ya Kombe la FA, ila tunachoshukuru nne tumeshinda na moja tumetoa sare kwa hilo tuna furaha sana," alisema kocha huyo ambaye kazi yake kubwa ni kuwafundisha makipa na kwa sasa anakaimu nafasi ya ukocha msaidizi akiwa benchini kwa sababu ya kadi nyekundu aliyopewa Selemani Matola katika mechi dhidi ya Azam FC, Ijumaa iliyopita.

"Tulichojiwekea kwa sasa ni kwamba kila mchezo ni pointi tatu kwa vyovyote vile itakavyokuwa, hakuna muda wa kupoteza tena, na mpira mzuri utakuja baadaye tutakapocheza kwenye viwanja rafiki na pia wachezaji wapya kuzoeana na wenzao," alisema Cadena.

Kocha Mkuu wa Geita Gold, Denis Kitambi, alisema amerishwa na kiwango walichoonyesha wachezaji wake katika mechi hiyo, akisema ni mapungufu machache tu yaliyojitokeza.

"Jambo la kwanza tulidili na mpira wa faulo, unajua kwa sasa Simba imebadilika, wanajua sana kutumia mipira iliyokufa, kona na faulo ni hatari sana, unaweza kuona mabao yao mengi tangu warejee tena kwenye ligi safari hii wanayafunga kwa staili hiyo, niwapongeze sana wachezaji wangu, waliweza kuwadhibiti katika mechi yetu hawakupata bao kwa njia hii," alisema.

Alizungumzia bao walilofungwa kuwa ni makosa ya wachezaji wake kuwaachia Simba kumiliki mpira kwa muda mrefu.

"Usipomiliki mpira na ukiruhusu muda wote unashambuliwa ni lazima utafanya makosa na ndicho kilichotokea, ni kwamba sisi hatukumiliki mpira kiasi cha kumpa mpinzani matatizo," alisema.

# Michezo

Nipashe

Jumatano Februari 14, 2024




Mbappe haeleweki hatima yake UK. 21

# Kilio Simba chasikika, Kayoko kikaangoni

●●● Bosi wa marefa awaomba radhi wadau wote wa soka kwa kilichotokea, asema...

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa Kamati ya Waamuzi, Nassor Hamduni, amewaambia wanachama na mashabiki wa Simba kuwa wamesikia kilio chao dhidi ya mwamuzi Ramadhani Kayoko na jambo hilo litakwenda kufanyiwa kazi na Kamati ya Nidhamu na anaweza kuadhibiwa iwapo itathibitika kuwa alikuwa na mapungufu kwenye uamuzi wake.

Ijumaa iliyopita baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Simba na Azam FC kumalizika, mashabiki wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao walifanya maandamano ndani ya uwanja wa CCM Kirumba, wakimshutumu mwamuzi huyo kwa kutochezesha mechi hiyo kwa haki, wakidai aliwanyima haki kwenye baadhi ya matukio na kuwafanya kutoka sare ya bao 1-1.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Hamduni aliwaomba radhi mashabiki na wadau wote waliokwazwa kwa njia moja ama nyingine kutokana na ufanyaji kazi wa waamuzi katika mechi za hivi karibuni ambazo zimeonekana kuwa na malalamiko mengi.

"Tumeyasikia, tunaheshimu kauli za mashabiki kwa sababu hao ndio wadau wetu wa soka na waswahili wanasema ndiyo wanaotuweka mjini, tumesikia na naomba kuweleza.

"Suala la kukataa mwamuzi si la mashabiki, viongozi au kamati yetu waamuzi, bali lipo kwenye kamati maalum ambayo inachunguza mwenendo wa waamuzi, na kama Kayoko ataonekana ana matatizo kwenye mechi aliyochezesha atachukuliwa hatua na si yeye tu, yeyote yule ambaye itabainika amevurunda, tunaomba mashabiki watulie wasubiri Kamati ya Nidhamu ambayo imeshajua hayo, watachukua hatua na sisi Kamati ya Waamuzi ikitufikia tutaridhika na maamuzi watakayochukua," alisema.

Mwenyekiti huyo amewaomba radhi mashabiki wa wadau wote wa soka ambao wamekwazwa na tukio hilo au lingine ambalo limesababishwa na kile ambacho wanaona waamuzi hawakutenda sawa.

"Napenda kuwapa pole wadau wote wa soka ambao wamekwazwa kwa njia moja ama nyingine kutokana na ufanyaji kazi wa waamuzi, sisi kama Kamati ya Waamuzi kwanza lengo letu kuwapanga waamuzi tu, si kwenda kuharibu mchezo, wala kuwanyima watu mabao au kuwapendelea watu, kwa hiyo sisi tutaendelea kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), kuhakikisha waamuzi wetu wanakuwa bora zaidi na hii ni kuwapa elimu na kueleza makosa yao yote," alisema.

INAENDELEA UK 23



Kayoko

# Gamondi aishtukia Simba SC, ageukia beki

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameonekana kushtushwa na kasi ya Simba katika mechi za hivi karibuni, hivyo ameanza kufanyia kazi safu yake ya ulinzi ambayo imekuwa ikiruhusu nyavu zao kutikiswa katika mechi mbili zilizopita.

Katika mbio hizo za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, Gamondi amesema inabidi afanye kazi ya ziada katika safu yake ya ulinzi, kwa kuwa timu wanayokimbizana nayo [Simba], inaonekana kiwango chao kuwa juu baada ya mapumziko ya mwezi mmoja na usajili mpya uliofanywa na 'Wekundu wa Msimbazi'.

Kikosi cha Yanga kimerejea jijini Dar es Salaam baada ya kumalizana na Tanzania Prisons kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-1, kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, hiyo ikiwa ni mechi ya pili kuruhusu bao.

Yanga waliruhusu bao katika mchezo dhidi ya Mashujaa FC kwa ushindi wa bao 2-1 wakiwa uwanja wa nyumbani, Azam Complex na hivi karibuni na Tanzania Prisons kwa kuibuka ushindi kama huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema licha ya kuvuna alama tatu katika michezo yao, lakini bado suala la kuruhusu bao katika michezo miwili anatakiwa kulifanyia




INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >